**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

# T A N G A Z O

## ILANI YA KUSUDIO LA KUTUNGA SHERIA – NDOGO

## [Chini ya Kifungu cha 155 [1] cha Sheria ya Serikali za Mitaa [Mamlaka za Wilaya] Sura 287]

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anawatangazia wananchi wote kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa Mamlaka iliyopewa chini ya **kifungu cha 155 [1]** cha Sheria ya Serikali za Mitaa [Mamlaka za Wilaya] Sura 287 inakusudia kutunga Sheria Ndogo zifuatazo;

1. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
2. Sheria Ndogo ya (Kodi ya Huduma) ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
3. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
4. Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii – Tiba Kwa Kadi) za Halmashauri za Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.

5. Sheria Ndogo Bodi ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
6. Sheria Ndogo za Kudhibiti Afya na Usafi wa Mazingira za Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
7. Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Ardhi Mazingira na Uchimbaji wa Madini) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
8. Sheria Ndogo za (Maendeleo na viwanda) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.
9. Sheria Ndogo za (Kudhibiti Mahudhurio ya Wanafunzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2018.

Kwa hiyo, Wananchi wote mnatangaziwa kushiriki katika kutunga Sheria Ndogo hizo kwa kutoa maoni, hoja au pingamizi vile unavyoona inafaa. Rasimu ya sheria husika imewekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na kwenye mbao za ofisi za vijiji na Kata zote za Halmashauri na kwenye ofisi za Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi, ili wananchi wasome au wapitie na kutoa maoni yao. Wananchi mnashauriwa kupita kwenye mbao za vijiji na kata kusoma na kukagua kila kifungu hususani nyakati za kawaida za saa za kazi kuanzia tarehe 10.01.2018.

Mwananchi atakayehitaji kudurufu nakala za rasimu za Sheria Ndogo husika ATARUHUSIWA, isipokuwa atafanya hivyo kwa kutumia gharama zake mwenyewe.

Hoja au pingamizi zozote kuhusu Sheria Ndogo hizi ziwasilishwe kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuanzia tarehe 10.01.2018 hadi tarehe 10.03.2018 kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya ya Chunya,
S.L.P. 73,
**CHUNYA.**

Tangazo hili limetolewa leo siku ya Jumatano tarehe 10/01/2018 na:-

……………………………………………….
SOPHIA JUMA KUMBULI
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**CHUNYA**

TANGAZO LA SERIKALI Na……………….la Tarehe ……………….

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya Kifungu vya 6 na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAEGESHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA, 2018

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kuanza kutumika | **1.** | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2018* na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | **2.** | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. |
| Tafsiri | **3.** | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:- |

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chombo cha usafiri" maana yake ni chombo cha moto ikijumuisha gari na pikipiki ya magurudumu matatu.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Maegesho Maalumu" maana yake ni eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa utaratibu uliowekwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi.

"Maegesho" maana yake ni sehemu iliyoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri isipokuwa stendi.

"Yadi" maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi

vyombo vya usafiri.

"Ushuru wa Maegesho" maana yake ni Ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anayeegesha chombo cha usafiri katika eneo lililoainishwa au kutambuliwa na Halmashauri.

Ushuru wa maegesho

**4.** (1) Halmashauri itatoza Ushuru wa maegesho kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatenga maeneo ya maegesho kwa vyombo vya usafiri vitakavyoegeshwa katika maeneo yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Sehemu za maegesho

**5.** (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi maeneo yote yaliyoainishwa ikiwa ni pamoja na pembezoni mwa barabara katika Halmashauri yatakuwa ni sehemu za maegesho ya vyombo vya usafiri;

(2) Itakuwa ni wajibu kwa mtu yeyote kuegesha chombo cha usafiri katika eneo lililoainishwa na Halmashauri.

Uegeshaji usioruhusiwa

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha magari aina yoyote au magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, kichochoro, mtaro au maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia.

Namna ya kutoza Ushuru wa Maegesho

**6.** (1) Ushuru wa maegesho utatozwa kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 12.00 jioni na utalipwa kwa kila siku au mwezi kadri Halmashauri itakavoona inafaa.

(2) Ushuru wa maegesho utalipwa na mtu yeyote mara tu anapoegesha chombo cha usafiri.

(3) Endapo mtu yeyote amelipa Ushuru wa Maegesho kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha chombo cha usafiri alicholipia katika eneo lolote lililoainishwa kwa ajili ya maegesho ndani ya Halmashauri kwa muda aliolipia.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi, chombo cha usafiri kinachomilikiwa na Serikali, Wanadiplomasia, Majeshi na magari ya taasisi au madhehebu ya dini na ya kubeba wagonjwa hakitatozwa Ushuru wa Maegesho.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**7.** (1) Afisa Mwidhiniwa atakua na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri kilichoegeshwa kwenye eneo ambalo halikuainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 7 kitaondolewa na kuhifadhiwa katika yadi ya Halmashauri au iliyoainishwa na Halmashauri.

(3) Halmashauri itakua na mamlaka ya kuuza chombo cha usafiri endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipa gharama za kuondoa chombo cha usafiri ndani ya kipindi cha siku 14 tangu tarehe ya kukamatwa.

Maegesho maalum

**8.** (1) Halmashauri inaweza kutenga eneo maalum la maegesho ya chombo cha usafiri na kiwango cha Ushuru wa maegesho kitakuwa kama ilivyoainishwa kwenye Sehemu A ya Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi muda wa kuegesha chombo cha usafiri katika maegesho maalum utapangwa kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Makosa

**9.** Itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote iwapo;-

(1) Atashindwa kulipa Ushuru wa Maegesho

(2) Ataegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaainishwa na Halmashauri.

(3) Ataosha chombo au kutengeneza chombo cha usafiri katika eneo la maegesho.

(4) Atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kutolipa Ushuru wa maegesho.

Adhabu

**10.** (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza.

Hati ya kufifilisha kosa

**11.** Mkurugenzi, Mwanasheria na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi watakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki mbili (200,000/=) iwapo mkosaji atakili kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa Ushuru wa Maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

SEHEMU A

Limetungwa chini ya kifungu cha 4(2)

USHURU WA MAEGESHO

| Na | Aina ya chombo cha usafiri | Ushuru kwa siku |
|---|---|---|
| 1. | Gari ya mizigo zaidi ya tani 5 | 2000/- |
| 2. | Gari ya mizigo chini ya tani 5 | 1500/- |
| 3 | Gari ndogo | 1000/- |
| 4 | Bajaji, guta, pikipiki | 500/= |

SEHEMU B

Limetungwa chini ya kifungu cha 8(1)

MAENEO YA MAEGESHO MAALUM

| Na | Aina ya chombo cha usafiri | Eneo la maegesho |
|---|---|---|
| 1 | Malori ya mizigo mchanga na kokoto | Msikitini jirani na kizimba cha maji na kwa wachina |
| 2. | Malori ya mizigo mingine. | Litapangwa na Halmashauri |
| 3. | Bajaji, guta, bodaboda | Litarasimishwa na Halmashauri |

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa chini ya kifungu cha 11

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya…………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi, kwamba mnamo tarehe……………ya mwezi……………..mwaka ……………………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru wa Maegesho ninachodaiwa pamoja na faini jumla shilingi…………………………..

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU BILA KUSHINIKIZWA NA MTU YEYOTE. HATA HIVYO NAKIRI SITORUDIA TENA KUTENDA KOSA KAMA HILO.

Maelezo haya nimeyatoa siku ya leo tarehe……………………………………………………

Saini…………………………………………

Jina…………………………………………..

Simu………………………………………….

Mbele ya:

Saini………………………………………..

Jina………………………………………..

Cheo………………………………………

TANGAZO LA SERIKALI Na …......…………. la tarehe ………..

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

**1.** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.* na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Mwanasheria au Afisa yeyote wa Halmashauri au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilya ya Chunya.

"Hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo ya bidhaa, kazi au Huduma katika mwaka wa fedha.

Sura 212

"Kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.

Sheria na. 7 ya mwaka 2011

"Kazi" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma.

"Kipindi cha Hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake kwa Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, Mwansheria wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

Sura 290

"Mkusanya kodi" maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya kodi.

"Ushuru wa Huduma" maana yake ni Ushuru unaotozwa au kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara yeyote kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri.

"Taasisi ya biashara"maana yake ni Taasisi inayofanya biashara, kazi au kutoa huduma kwa lengo la kupata faida.

"Tawi la kampuni"maana yake ni tawi la kampuni lililosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.

"Ukokotoaji" maana yake ni namna ya kuandaa kiasi cha Ushuru wa Huduma kinacholipwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa Ushuru wa Huduma

**4.** Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kwa kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara, au mfanyabiashara kwa kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri ukiondoa Kodi ya ongezeko la thamani na Kodi ya mlaji (VAT).

Uwasilishaji wa taarifa kuhusu shughuli za kibiashara

**5.** (1) Mkurugenzi kwa taarifa ya kimaandishi, anaweza kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za biashara zikionyesha kiasi cha thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa, au kuuzwa kibiashara, taarifa ya fedha katika kipindi kisichozidi siku ishirini na moja tangu tarehe ya taarifa hiyo.

(2) Kila mfanyabiashara atawasilisha kwa Halmashauri taarifa sahihi za hesabu za mauzo ya kila mwezi husika na atalipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa viwango vitakavyotokana na hesabu hizo na kwa wafanyabiashara wasio na vitabu vya hesabu watakokotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Mkurugenzi anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu mfanyabiashara anayepaswa kulipa Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumika kama taarifa sahihi.

Uwezo wa kuingia kwenye jengo

**6.** (1) Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa muidhiniwa au Wakala kuingia kwenye jengo au eneo la taasisi ya kibiashara au la mlipa au mkusanya kodi yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanyaji kodi hiyo.

(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa afisa muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

Ukokotoaji wa Ushuru wa Huduma

**7.** (1) Halmashauri kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi itakokotoa na kutoza Ushuru wa Huduma

(2) Halmashauri itamtaka mlipa kodi alipe ushuru uliotokana na hesabu zilizokokotolewa na Halmashauri..

Uwasilishaji wa taarifa

**8.** Kila mlipa au mkusanyaji kodi ya huduma atatakiwa kutoa na kuwasilisha hesabu na kulipa kodi anayotakiwa katika muda anaopaswa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda kama itakavyokuwa imeelezwa na Kamishna wa Kodi ya Forodha na kodi ya mlaji;

(b) Wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa kodi kama itakavyokuwa imeelekezwa na Kamishna wa Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa Kodi ya mlaji au VAT na

(c) Wengine watalipa katika awamu nne kila baada ya miezi mitatu kupita au kulipa zote kwa awamu moja kwa mkupuo

Makadirio ya kiwango cha mlipa kodi

**9.** Iwapo mlipa kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa mapato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi anafikiri kwamba Mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi mwaka huo anaweza kwa kadiri anvyoona, kuamua

kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa kodi anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa kushindwa kwake uwasilishaji hesabu hizo.

Muda wa kulipa kodi

**10**. (1) Kodi iliyotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi italipwa ndani ya kipindi cha siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

(2) Mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatozwa riba ya 2% kwa mwezi au shilingi 50,000/= kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.

(3) Mtu yeyote atawasilisha taarifa za uongo au kuficha baadhi ya hesabu kwa lengo la kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi, mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya kodi ya asilimia 50 ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha kodi halisi.

Jumla ya riba kutozwa kwenye kodi isiyolipwa

**11**. (1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya 20% kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi inayodaiwa.

(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama kodi inayolipwa pamoja na mlipa kodi huyo.

Uteuzi wa wakala

**12**. (1) Halmashauri inaweza kuteua Kamishna wa Kodi ya forodha au kodi ya mapato au wakala kutathmini na kukusanya kodi ya huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata kodi pamoja na madeni yake.

(2) Mlipa kodi, mkusanya kodi au wakala yeyote akishindwa kuwasilisha kodi yake au ya mlipa kodi atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kuwajibika kulipa kodi kama hiyo kama vile ndiye mlipa kodi ya Halmashauri na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipaji kodi husika.

Makosa

**13**. (1) Mtu yeyote yule atakuwa ametenda kosa iwapo bila sababu za

msingi:-

(a) Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli

(b) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;

(c) Atashindwa kutunza kumbukumbu, kitabu au hesabu za mauzo yake;

(d) Atashindwa kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi.

(e) Akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi

(f) Akitoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi

(g) Akiandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu;

(h) Atamzuia au atajaribu kumzuia afisa muidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

**14**. (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kuanzia shilingi laki moja hadi laki tatu na haitazidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza.

| | | |
|---|---|---|
| Kufifilisha kosa | **15** | Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki moja hadi laki tatu na haitazidi shilingi laki tatu (300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la I la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa Ushuru wa Huduma pamoja na faini anayodaiwa. |
| Kufutwa kwa sheria ndogo | **16** | Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya (Ushuru wa huduma) 2015 zilizotangazwa kwenye gazeti la Serikali Na 484 la tarehe 30/10/2015 zimefutwa. |

JEDWALI LA I

KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa Chini ya kifungu cha 15

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya……………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwnasheriawa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi kwamba mnamo tarehe……………ya mwezi……………..mwaka ……………………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, Mwnasheriawa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru wa Huduma ninachodaiwa pamoja na faini jumla shilingi…………………………… ambapo naahidi kulipa siku ya tarehe…………………………………………

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………………ya mwezi…………………Mwaka………………………..

Jina…………………………………..

Saini………………………………….

Mbele ya:

Jina………………………………………..

Cheo………………………………………

Saini………………………………………

TANGAZO LA SERIKALI Na. ……….. la Tarehe …………………………

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

*Imetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (KUIMARISHA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA ZA MWAKA 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

**1.** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kuimarisha Afya Na Usafi Wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lilila chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"Ada ya uzoaji taka"maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma ya uzoaji taka;

“Afisa mwidhiniwa” maana yake ni Mganga Mkuu wa Wilaya, Afisa Mazingira, Afisa Afya, Mwanasheria wa Halmashauri, Daktari wa binadamu, Daktari wa Mifugo, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Mtendaji wa kijiji au Afisa mwingine yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Afya” maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na sio tu kuwa na ugonjwa au ulemavu;

“Chakula” maana yake ni ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa hii ni pamoja na:-

(a) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula kama binzari n.k
(b) kitu chochote kinachoongeza ladha;
(c) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

“Chanzo cha maji” maana yake ni mito, bwawa, lambo, kisima au maji yapatikanayo chini ya ardhi;

“Choo” maana yake ni choo cha maji (kuvuta) au cha shimo;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

“Idhini” maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mkazi yeyote wa Halmashauri anayekusudia kufanya jambo fulani katika maeneo ya Halmashauri;

“Kaya”maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo,au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

“Kero” maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote au kinatumika au kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

(a) harufu mbaya na ya kuudhi;
(b) hatari kwa viumbe au maisha ya binadamu;

(c) Kelele za aina yoyote ile kama sauti kubwa ya redio au mziki.
(d) Magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, inzi, panya na viumbe wenye madhara.
(e) Kero ni pamoja na mavazi yasiyofaa yanayoonyesha maungo ya sehemu za siri mfano sketi fupi, kuvaa suruali chini ya matako nk

"Maduka" maana yake inajumuisha maduka ya bidhaa za nguo, vyakula, madawa, vifaa vya ujenzi na vioski, bucha za nyama, pamoja na maduka mengine yaliyopo katika eneo la Halmashauri ambayo hayakutajwa;

"Majumba ya starehe" maana yake inajumuisha kumbi za dansi, bar, grocey, majumba ya kuonesha video na vilabu vya starehe;

"Mdudu" maana yake ni mdudu yoyote ambaye anaweza kuharibu vyakula, bidhaa, vinywaji au kuathiri mazingira kiasi cha kusababisha magonjwa au kudhuru afya ya binadamu au jamii kwa ujumla na ni pamoja na mbu na inzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Mwanasheria wa Halmashauri, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi au Afisa mwingine yeyote atakayetekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mlipuko wa ugonjwa" maana yake ni maradhi au mlipuko wa maradhi ya aina yoyote ile ambao ni hatari kwa afya ya binadamu au jamii kwa ujumla, unaweza kujitokeza katika eneo lolote na kwa wakati wote kama vile kipindupindu.

"Mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye anamiliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, hotel au pub au rounge, elution, plant ya kuchenjua dhahabu,, chumba cha kuchomea dhahabu, kumbi za starehe, bar, grovery, gari, gereji, sheli, kalakana, kiwanda, shule na Zahanati, mpangaji, wakala wa mpangishaji nyumba au jengo na makazi yoyote katika mtaa au kijiji endapo mazingira husika ni mtaa au kijiji au barabara za mitaani au kijijini;

"Nyumba za vyakula" maana yake ni hoteli, mgahawa, bar, grocery, kilabu cha pombe za kienyeji, magenge ya chakula na inajumuisha mahali popote panapouzwa matunda, kahawa, maziwa, juisi, chai, soda, chipsi, mishikaki, karanga, nyama choma na vyakula vinavyopikwa au visivyopikwa;

"Pipa la taka" maana yake ni chombo chenye mfuniko cha kuhifadhia takataka kabla hazijatupwa au kuchomwa moto au kufukiwa shimoni;

"Shimo" maana yake ni shimo au ardhi iliyochimbwa kwa ajili ya kumwagia au kutupia uchafu au kupokea na kutia maji machafu;

"Taka" kama ilivyo katika Sheria za usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, au uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira amabayo yanajumuisha taka;

"Taka Ngumu" maana yake ni aina zote za taka zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani lakini haihusishi maji taka au taka miminika.

"Uchafu hatari" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia kwa binadamu au mazingira;

"Wanyama" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda pamoja na wanyama wengine wafugwao kama vile mbwa na farasi

Kukusanya na kuhifadhi taka majumbani

**4.** (1) Itakuwa ni wajibu wa mtu yeyote anayemiliki nyumba au mpangaji wa nyumba ya kuishi au ya biashara kuweka chombo cha kuhifadhia taka chenye ukubwa unaotosheleza na kiwe na mfuniko unaofaa na kuhakikisha kwamba kinatumika na kuhakikisha kwa

(a) Kufagia na kuondoa uchafu au malundo ya uchafu na

kuweka safi eneo lote la nyumba yake

(b) Kutunza katika hali ya usafi vichochoro vyote vinavyomzunguka.

(c) anapanda miti ya kivuli na matunda kwa ajili ya kuboresha mazingira katika eneo lake;

(d) anazibua mifereji ya maji machafu inayozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo lake la mara inapokuwa imeziba;

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka katika chombo cha kuhifadhia taka kitu kinachoweza kuleta madhara kwa binadamu au kusababisha moto au mlipuko.

(3) Taka zote zilizohifadhiwa majumbani zihifadhiwe ndani ya ua mpaka zitakapochukuliwa au mhusika azipeleke mwenyewe dampo liliotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

Kuhifadhi taka kwenye magari ya abiria

**5.** (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa chombo cha usafiri linalosafirisha abiria katika eneo la Halmashauri kuwa na chombo cha kuhifadhia taka na kuhakikisha kila abiria anatupa taka zake humo.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mmiliki iwapo abiria aliyeko ndani ya chombo cha usafiri wake atatupa kitu chochote barabarani au sehemu yeyote katika eneo la Halmashauri.

Ada ya usafi na uzoaji taka

**6.** (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya au mwenye jengo lolote liwe la biashara au vinginevyo litatozwa ada ya usafi na uzoaji taka kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la kwanza Sehemu A la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 28 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa muidhiniwa au wakala ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejesta ya wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji taka atakuwa hajalipa ada ya mwezi kufikia tarehe 10 ya mwezi unaofuata atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyozidi asilimia hamsini (50%) ya ada anayostahili kulipa.

(4) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Udhibiti wa kelele au mtikisiko

**7.** Itakuwa ni marufuku kusababisha utoaji wa kelele majumbani, sehemu za burudani, bar, club, grocery, sokoni, barabarani bila kibali, ofisini, mahakani au kwenye baraza la kata au mtikisiko

kwenye maeneo ya ujenzi, mitambo, magari pamoja na vipaza sauti kwenye shughuli za viwanda na biashara au kwenye plant na elution za uchomaji wa madini.

Wajibu wa kushiriki shughuli za usafi wa mazingira

**8.** (1) Halmashauri imetenga kila siku ya Jumamosi ya mwisho ya kila mwezi kuwa ni siku ya wananchi kushiriki usafi katika maeneo yanayopangwa na Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha anashiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku iliyopangwa na mwananchi yeyote atakayekataa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Wajibu wa kutumia Vyoo

**9.** (1) Ni wajibu wa mtu yeyote au mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

(a) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka katika kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani.

(b) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayemiliki shule, bweni, kiwanda, mgahawa, hoteli, bar, grocery, elution, plant ya uchenjuaji, maeneo yaliyofungwa makarasha au eneo lolote lenye mkusanyiko mkubwa wa watu au sehemu za burudani kuweka vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanawake na wanaume na atahakikisha kuwa vyoo hivyo vina mwanga na hewa ya kutosha na maji kila wakati.

Ujenzi wa vyoo vya umma

**10.** (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu, kampuni au taasisi kujenga vyoo vya umma (public toilet) katika maeneo ambayo itaona inafaa kufanya hivyo.

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na mjenzi na vitakuwa ni vya kulipia kwa gharama zitakazoainishwa katika mkataba kati ya Halmashauri na wakala atakayeteuliwa kusimamia vyoo hivyo.

Ilani ya kujenga choo

**11.** (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa mwidhiniwa atatoa ilani ya siku

thelathini kwa mwenye nyumba au mpangaji kumtaka arekebishe hali hiyo.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga choo chochote ambacho kitaonekana kichafu au cha kuhatarisha maisha ya binadamu na hakitaruhusiwa kutumika mpaka Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara mpaka mmiliki wake atakapokuwa ametimiza maelekezo aliyopewa.

Ilani ya kuondoa kero

**12.** (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji na au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Utiririshaji maji taka ya viwandani, elution au plant na maeneo ya makarasha yenye harufu na madhara

**13.** Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote:

(1) Kuendesha karasha, elution au palanti ya madini, gereji au karakana, kiwanda kinachotoa maji taka bila ya kudhibiti yasisababishe madhara kwa watu wengine.

(2) Kuruhusu maji taka toka viwandani, makarashani, aelution aua planti, bara grocery au mgahawa au eneo lolote kuingia katika vyanzo vya maji safi, maeneo ya wazi au ardhini bila kudhibitiwa.

(3) Kusababisha harufu yenye madhara inayotokana na shughuli zinazofanyika katika eneo hilo mfano kupitia elution za uchomaji wa madini.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua

**14.** Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi takataka au vitu vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakiksha mfereji huo unakuwa safi siku zote.

Mimea mirefu kutooteshwa mjini

**15.** Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri. Mimea mirefu maana yake isiyozidi futi tatu mfano mahindi ni mimea mirefu haitakiwi.

Ufugaji mjini

**16.** Ufugaji unaoruhusiwa ni ufugaji wa ndani ya zizi (zero grazing) kwa kuzingatia idadi ya mifugo inayoruhusiwa kulingana na ukubwa wa eneo au katika maeneo yaliyotengwa kama malisho ya mifugo.

Wajibu wa wafugaji

**17.** Ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba:-

(a) Mifugo yake haizururi ovyo mitaani, barabarani au kuchungwa katika maeneo yasiyoruhusiwa.

(b) Sehemu anayotumia kufugia inakuwa katika hali ya usafi wakati wote.

(c) Anakusanya uchafu wowote utokanao na mifugo kama vile kinyesi, manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupwa kwenye dampo au ghuba au kupelekwa shambani kama mbolea.

(d) Mifugo yake haiharibu miti, mazao au maua katika bustani za Halmashauri au mali ya mtu mwingine yeyote.

(e) Mifugo yake inapatiwa chanjo kila inapohitajika ili kuzuia magonjwa mbalimbali.

(f) Kusafirisha mifugo kutoka eneo moja la Halmashauri kwenda eneo jingine kwa kibali maalum cha Halmashauri.

(g) Mifugo haipitishwi kwenye barabara.

Udhibiti wa mifugo

**18.** (1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kuamuru mifugo ihamishwe ikiwa ufugaji huo unakinzana na masharti ya Sheria Ndogo hizi pamoja na Sheria ya Mipango Miji na kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo husika.

(2) Halmashauri itakamata mfugo au mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika maeneo ambayo yasiyoruhusiwa kuchungia mifugo.

(3) Mifugo au mfugo uliokamatwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 17,18 cha Sheria Ndogo hizi utalipiwa faini pamoja na gharama za utunzaji.

Faini ya mifugo itakuwa:

a) Ng’ombe…..shilingi 50,000/= kwa kila Ng’ombe
b) Punda ……..shilingi 40,000/=kwa kila Punda
c) Mbuzi na Kondoo shs 30,000/=kwa kila Mfugo
d) Nguruwe…..shilingi 20,000/= kwa kila Nguruwe
e) Wanyama wengine….15,000/= kwa kila mnyama

(4) Endapo mwenye mfugo au mifugo iliyokamatwa hataonekana ndani ya muda wa siku tatu (3) tangu kukamatwa kwa mfugo

au mifugo hiyo Mkurugenzi atauza mfugo au mifugo hiyo kwa njia ya mnada baada ya kupata kibali cha Mahakama.

(5) Baada ya mauzo Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada, ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mfugo au mifugo na endapo hataonekana ndani ya siku saba fedha hizo zitaingizwa kwenye vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mfugo au mifugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

(7) Mbwa watakaozurula na ambao hawatachanjwa watauwawa kwa kupigwa risasi. Baada ya kuuawa mmiiliki akipatikana atalipa faini ya shilingi 50000/= kwa kosa la kuwaacha mbwa wanazurula ovyo lakini kuanzia saa moja jioni hadi saa kumi na mbili asubuhi mbwa watakuwa huru kwa ajili ya ulinzi.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

**19.** (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza kuchoma, kupima, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yeyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya kwa kupata kibali cha Afisa Afya wa Halmashauri na leseni ya biashara.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwa vyakula hivyo vinahifadhiwa kwa namna inayozuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya kwa binadamu.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwa juu ya meza au kabati.

Biashara ya matunda au miwa

**20.** (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda au miwa kuhakikisha ana chombo maalum cha kuhifadhi mabaki ya maganda au matunda.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara ya matunda au miwa, mbogamboga, nyanya na samaki katika sehemu zisizoruhusiwa na Halmashauri au kuuza nje ya soko.

Machinjio na maduka ya nyama

**21.** (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kuwa duka lake

(a) Jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe.

(b) Lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama

(c) Lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu ya mizani,
(d) Kuna pipa la kuhifadhia takataka
(e) Muuzaji ana vazi jeupe pamoja na apron nyeupe na kofia
(f) Muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita

Kuuza na kuchinja nyama mahali pasiporuhusiwa

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote au kuwa na duka la nyama katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

**22.** (1) Afisa muidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mujumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote ile kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu kama vile kipindupindu..

Ukamataji wa vyombo vilivyotumika kuhifadhia chakula

(2) Vyakula, vyombo na vifaa vingine vyovyote vitakavyokamatwa baada ya kutolewa amri ya kuzuia kufanyika kwa shughuli hiyo ambavyo vitakuwa vimetumika kutunzia, kubebea, kuhifadhia na kusafirishia vitaharibiwa na Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea wakati wa utekelezaji wa amri hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayekataa kutii amri iliyotolewa atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa Halmashauri

**23.** (1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya kutupa takataka itakayojulikana kama dampo au ghuba na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kijamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa na vitongoji baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

(3) Kumchukulia hatua za kisheria mkazi yeyote atakayekataa kutekeleza maagizo ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Ada ya ukaguzi wa afya

**24.** (1) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara

kwa viwango vitakavyoainishwa katika jedwali la kwanza sehemu B la Sheria Ndogo hizi

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya 50% ya kiwango anachodaiwa.

Mkurugenzi kuteua Mkaguzi

**25.** (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote au Afisa mwidhiniwa kuwa Mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri.

(2) Mkaguzi atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa kiasi kinachoanzia shilingi elfu hamsini hadi laki tatu lakini hakitazidi shilingi laki tatu kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kuchafua mazingira au kutupa takataka mahali popote pasiporuhusiwa.

Makosa

**26.** Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-

(1) Atamzuia au kujaribu kumzuia afisa mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashuri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataaa au kukwepa kulipa Ada.

(4) Atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri.

(5) Atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani.

(6) Ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea au madini ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu.

(7) Atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo

yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji.

(8) Ataenda haja Ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni au mahali popote ambapo siyo chooni.

(9) Atajenga jengo, plant au elution ya madini, karakana, kiwanda, gereji, shule, zahanati, club, bar, hotel, ukumbi wa mazoezi jimu, sheli bila kibali au bila kufuata taratibu za mipango miji.

(10 Atasababisha kuchoma moto eneo la msitu wowote

Adhabu

**27.** (1) Mtu yoyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kuanzia shilingi elfu hamsini hadi laki tatu na haitazidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza

Kufifilisha kosa

**28.** Mkurugenzi au Mwanasheria wa Halmashauri, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi watakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi faini kuanzia shilingi elfu hamsini hadi laki tatu na haitazidi shilingi laki tatu (300,000/=) iwapo mkosaji atakili kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa Ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa sheria za awali

**29** Sheria Ndogo ya Usafi wa mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2015 Tangazo la serikali namba 487 la tarehe 30/10/2015 na Sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya (Hifadhi ya Mazingira) 2015 Tangazo la serikali namba 486 la tarehe 30/10/2015 zote kwa pamoja zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

SEHEMU A

*Chini ya kifungu cha 6(1)cha sheria ndogo hizi*

ADA YA UZOAJI TAKA KATIKA MAJENGO SHUGHULI ZA MADINI

| Na. | Eneo | Ada kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Kaya moja | 1,000.00 |
| 2. | Maduka la rejareja | 3,000.00 |
| 3. | Mashine ya kukamua mafuta ya alizeti | 5,000.00 |
| 4 | Maduka la jumla | 5,000.00 |
| 5 | Migahawa(Restaurant) | 3,000.00 |
| 6 | Mashine za kukoboa/kusaga | 5,000.00 |
| 7 | Vilabu vya pombe za kienyeji, baa, grocery, | 5,000.00 |
| 8 | Mama lishe/Baba lishe, Nyama choma/chipsi inayojitegemea | 3,000.00 |
| 9 | Elution, Plant ya uchenjuaji wa madini, gereji, Viwanda vya uselemala na mashine za mbao, karakana | 10,000.00 |
| 10 | Bucha(Maduka ya Nyama, samaki) | 5,000.00 |
| 11 | Nyumba za kulala wageni | 5,000.00 |
| 12 | Saluni (Ususi/Vinyozi) | 3,000.00 |
| 13 | Gereji | 10,000.00 |
| 14 | Godown (Ghala) | 7,000.00 |
| 15 | Kituo cha kuuza mafuta(Filling station) | 10,000.00 |
| 16 | Ofisi za Taasisi mbalimbali | 10,000.00 |
| 17 | Hoteli | 10,000.00 |
| 18 | Stoo za mkaa | 5,000.00 |
| 19 | Mafundi kushona nguo | 3,000.00 |
| 20 | Mafundi vyuma(wahunzi) | 10,000.00 |
| 21 | Kumbi za starehe,sinema | 10,000.00 |
| 22 | Majengo ya kuoshea magari/pikipiki | 5,000.00 |
| 23 | Zahanati/kituo cha afya au hospitali | 20,000.00 |
| 24 | Majengo mengine yasiyotajwa | 20,000.00 |

SEHEMU B

*Chini ya kifungu cha 24 Cha sheria Ndogo hizi*

ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Na | Aina ya biashara | Ada kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1 | Baa na maduka ya vinywaji (groceries), bucha | 5000.00 |
| 2 | Migahawa na mama lishe | 2000.00 |
| 3 | Nyumba za wageni(Guest House) na hoteli | 10,000.00 |
| 4 | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000.00 |
| 5 | Majengo ya elution, plant na vyumba vya madigala | 10,000.00 |
| 6 | Majengo mengine ya biashara | 7,000.00 |

SEHEMU C

*Chini ya kifungu cha 11cha sheria Ndogo hizi*

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo za (Kuimarisha Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.

AYA YA I

Ndugu……………………………………….simu……………………………….waKitongoji cha………………………Kijiji……………………..……….Kata……………………... Tarafa……………………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe………Mwezi………………Mwaka……………katika nyumba yako ya biashara/kuishi/kutolea Huduma*/Namba iliyopo eneo la ……………...…………………..katika kitongoji/Mtaa*………………Kijiji cha………………. Kata ya…………………………………

Imekuwa haina choo/choo kimejaa/kimeharibiwa*, hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:

1. ……………………………………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………………………………
4. …………………………………………………………………………………………...

AYA YA II

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika aya ya I ya ilani hii.

AYA YA III

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe……………………….endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

Saini……………………………………………..

Majina………………………………….............

Simu…………………………………………..

Aya hii-Mtu aliyekosa kama amepatikana wakati wa kutoa ilani

SHAHIDI ALIYETHIBITISHA NI :

Saini…………………………………

Majina……………………………..

Simu………………………………...

Tarehe……………………………...

IMETOLEWA NA :

Saini …………………………….

Majina ………………………….

Wadhifa…………………………..

Tarehe……………………………...

*Futa lisilohusika

SEHEMU D

*Chini ya kifungu cha12*

ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria Ndogo za (Kuimarisha Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya 2018.

AYA YA I

Ndugu……………………………………….simu………………………………waKitongoji cha……………………….Kijiji……………………..……….Kata……………………...
Tarafa……………………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe………Mwezi………………Mwaka……………katika nyumba yako ya biashara/kuishi/kutolea Huduma*/Namba iliyopo eneo la ……………...…………………..katika kitongoji/Mtaa*………………Kijiji cha………………. Kata ya…………………………………
Tumekuta machukizo/kero/uchafu*, hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………………………...

AYA YA II

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa:

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………………………...

AYA YA III

Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ya II ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.
Saini…………………………………………..Majina……………………………….............Simu…
……………………….Aya hii-Mtu aliyekosa kama amepatikana wakati wa kutoa ilani

SHAHIDI ALIYETHIBITISHA NI :
Saini…………………………………
Majina………………………………..
Simu………………………………...
Tarehe……………………………...

IMETOLEWA NA :
Saini …………………………….
Majina ………………………….
Wadhifa…………………………..
Tarehe……………………………...

*Futa lisilohusika

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 27)cha sheria ndogo hizi*

Mimi……………………………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya………………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwanasheria wa Halmashauri, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi kwamba mnamo tarehe……ya mwezi……………..mwaka ………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Kuimarisha Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, Mwanasheria wa Halmashauri, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninachodaiwa pamoja na faini. Nitalipa jumla shilingi………………………………..tarehe…………………………….

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………………ya mwezi…………………Mwaka……………………………...
Saini…………………………………………Jina……………………………………………
Simu ya Mkononi……………………………………………………………………………….

Mbele ya:

Saini………………………………………..

Majina………………………………………

Wadhifa……………………………………

TANGAZO LA SERIKALI Na …......…………. la tarehe ………..

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (URATIBU WA ELIMU NA UDHIBITI WA MAHUDHURIO YA WANAFUNZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

**15.** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo za (Uratibu wa Elimu na Udhibiti wa Mahudhurio ya Wanafunzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018* na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**16.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Tafsiri

**17.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

**“**Afisa Mwidhiniwa**”** maana yake ni Afisa yeyote wa umma au Mwalimu au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

**“**Afisa Mtendaji**”** maana yake ni Afisa wa kata au kijiji aliyeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi za Afisa Mtendaji kwenye eneo la kata ama kijiji.

**“**Baraza la kata” maana yake ni Baraza la kata lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata.(Ward Tribunal)

**“**Elimu” maana yake ni elimu ya shule za msingi na hule za Sekondari.

**“**Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Halmashauri za Vijiji vya Wilaya ya Chunya.

**“**Mkurugenzi**”** maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi ikiwa ni pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi.

**“**Mtendaji Mkuu” maana yake ni mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi.

**“**Mzazi” maana yake ni Mama, Baba au mtu yeyote ambaye anabeba dhamana ya mzazi akiwa kama mlezi wa

mwanafunzi.

“Mahudhurio” maana yake ni kuhudhuria ratiba ya masomo ya shule kama yalivyopangwa na uongozi wa shule.

“Mkuu wa Shule” maana yake ni Headmaster au Mwalimu Mkuu wa Shule za Msingi.

“Mwanafunzi” maana yake ni mtoto aliyeandikishwa kwenye shule yoyote ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na anatambulika kama mwanafunzi.

“Mwanasheria” maana yake ni mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

“Shule” maana yake ni shule zote za Msingi na Sekondari zilizosajiliwa na zilizopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Wajibu wa wazazi na walezi

**18**. Itakuwa ni wajibu wa kila Mzazi na mlezi kuhakikisha kwamba mwanafunzi anahudhuria vipindi vyote vya masomo ya shule kama ilivyopangwa na uongozi wa shule na atahakikisha anampatia mahitaji yake yote ya msingi.

Wajibu wa mwanafunzi

**19**. (1) Kila Mwanafunzi atahakikisha anahudhuria masomo na vipindi vyote shuleni kwa kuzingatia ratiba na maelekezo ya walimu wake.

(2) Kila Mwanafunzi atahakikisha anafuata na kuzingatia kanuni taratibu zote za shule

(3) Kila Mwanafunzi atahakikisha kwamba anawahi darasani kwa ajili ya vipindi na anajizuia na uvutaji sigara, bangi, kujiingiza kwenye mapenzi mambo ya uizi.

Wajibu wa mwalimu

**20**. (1) Kila mwalimu anayehusika na mahudhurio ya wanafunzi atahakikisha anachukua rekodi ya mahudhurio ya mwanafunzi na kutunza kitabu cha kumbukumbu.

(2) Kila Mwalimu kwenye kipindi chake darasani atahakikisha anafuatilia mahudhurio ya wanafunzi wake wanaostahili kuwepo kwa wakati huo.

Wajibu wa kila Mwanajamii

**21**. (1) Kila Mtu kwenye jamii yake anawajibu wa kutoa taarifa kwenye uongozi wa kijiji au kata iwapo anazo taarifa au amegundua kuwa mwanafunzi anatoroka vipindi au anazagaa mitaani bila idhini ya

uongozi wa shule.

(2) Kila mwanajami au mwananchi atahakikisha kwamba anashiriki kuweka miundombinu rafiki inayomuwezesha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote shuleni.

Katazo la ushiriki wa baadhi ya kazi kwa wanafunzi wenye umri mdogo

**22**. Wanafunzi wenye umri chini ya miaka kumi na tano hawataruhusiwa kushiriki au kushirikishwa kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kushiriki au kufanyishwa kazi za machimbo ya madini aina yoyote ikiwa ni pamoja na kuajiriwa kwenye mitambo ya uchenjuaji

(b) Kushiriki kwenye shughuli za kilimo cha tumbaku kama kibarua wa kazi hiyo

(c) Kushiriki au kushirikishwa kuuza vileo vya aina yoyote

(d) Kushiriki au kushirikishwa kwenye shughuli za kuchunga mifugo.

Kuzuia kukaa au kufanya kitu na mwanfunzi anayetakiwa kuwa shuleni

**23**. Hakuna mtu atakayeruhusiwa kwa namna yeyote:-

(a) Kukaa na mwanafunzi mwenye umri wa kuanza shule bila kuhakikisha anaandikishwa

(b) Kumzuia mwanafunzi kwenda shule kwa kumpatia kazi yoyote

(c) Kumwoza mwanafunzi

(d) Kukaa na mwanafunzi kwa kumuweka kama kimada

(e) Kumtuma mwanafunzi kufanya chochote kwenye maeneo yanayouzwa pombe.

(f) Kumkatisha mwanafunzi masomo

(g) Kumchumbia mwanafunzi

Hatua za kuzingatia iwapo Mwanafunzi anaonesha tabia ya utoro shuleni

**24**. (1) Mzazi au mlezi ili kudhibiti tabia ya utoro kwa mwanafunzi anayeonesha kugundulika ni mtoro shuleni atahakikisha anachukua hatua zifuatazo:-

a) Anamwonya Mwanafunzi.

b) Anatoa taarifa haraka kwenye uongozi wa kijiji na uongozi wa shule ikiwezekana kituo cha polisi kilichopo jirani.

(2) c) Anamnyima fursa ya kumshirikisha kwenye kazi zozote mwanafunzi ambaye ni mtoro.

(3) Uongozi wa shule utachukua hatua za kinidhamu kwa mwanafunzi atakayethibitika kuwa ni mtoro.

Uongozi wa vijiji/ unaweza kuweka utaratibu hatua zingine kuhusu mwanafunzi mtoro.

Kudhibiti vishawishi vya utoro kwa wanfunzi mashuleni

**25**. (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kumuingiza mwanafunzi kwenye kumbi za starehe kwa ajili ya kufanya starehe yoyote.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kumpatia kileo chochote mwanafunzi au kumuhusisha na biashara ya madini au tumbaku.

(3) Kumhusisha na shughuli za kuendesha bodaboda mwanafunzi yeyote itakuwa ni kosa

Likizo za wanafunzi

**26**. (1) Wakati wa likizo na kabla ya miezi sita ya matokeo ya mtihani wa mwisho mwanafunzi hataruhusiwa kufanya jambo lolote lililokatazwa kwenye sheria hii.

(2) Mzazi au mlezi kwa sababu au kisingizio chochote akimchelewesha mwanafunzi kufungua shule baada ya likizo kuisha atahesabika kwamba amefanya au amesababisha utoro kwa hiyo atatakiwa kuchukuliwa kwa makosa hayo kwa kushitakiwa kwenye baraza la kata au mahakama ya mwanzo iliyopo jirani

Makosa

**27**. (1) Mtu yeyote yule Mzazi au Mlezi au mtu mwingine yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo bila sababu za msingi:-

(i) Atakaa na mtoto nyumbani mwenye umri wa kwenda shule badala ya kumpeleka shule.

(j) Atashiriki kumtorosha mwanafunzi shuleni

(k) Atamzuia mwanafunzi kutoendela na masomo kwa kisingizio chochote.

(l) Atamwajiri mwanafunzi kwenye ajira zote hatarishi za machimbo au uchenjuaji wa madini, kilimo cha tumbaku au ajira ya kuuza vileo na kuendesha bodaboda au kuchunga ng’ombe

(m) Akimfungisha ndoa mwanafunzi

(n) Akimchumbia mwanafunzi.

(o) Akimwozesha mwanafunzi.

(p) Akisingizia kumfuta shule mwanafunzi

(q) Akimkarisha mwanafunzi kama kimada

(r) Akimtongoza mwanfunzi kwa namna yoyote ya kutaka kufanya mapenzi

Adhabu

**28**. (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza na atashitakiwa kwenye baraza la kata au mahakama yoyote.

Kufifilisha kosa

**15** Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mmlaka ya Mji mdogo wa Makongolosi na Afisa Elimu watakuwa na uwezo wa kumwagiza Mratibu wa kata au Mkuu wa shule kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki tatu (300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la I la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa gharama zingine za ukamataji kama zilitumika.

JEDWALI LA I

KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa Chini ya kifungu cha 15

Mimi…………………………………………….nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya……………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, Mratibu Elimu wa kata au Mkuu wa shule kwamba mnamo tarehe………………………………………………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Uratibu wa elimu na udhibiti wa mahudhurio ya wanafunzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.

Nakiri kwamba nimetenda kosa la…………………………………………………………ambalo linahusiana na mwanafunzi(jina)………………………………………………………….kwa hiyo kutokana na makosa hayo niko tayari kuadhibiwa kwa kulipa faini na gharama zingine zilizotumika kiasi cha jumla shilingi…………………………………………………………………

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YOTE NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU NA SIJASHINIKIZWA NA MTU YEYOTE. HATA HIVYO NITAHAKIKISHA MWANFUNZI HUYO ANAHUDHURIA MASOMO NA VIPINDI VYOTE KWA MUJIBU WA RATIBA YA SHULE

Maelezo yametolewa leo tarehe…………………………………………………..……….

Saini yangu………………………………………………..Simu yangu………………….

Majina yangu………………………………………………………………………………

Mbele ya:

Saini yake…………………………………………………………....

Majina yake………………………………………………………….

Cheo Chake………………………………………………………….

Simu yake………………

TANGAZO LA SERIKALI NA …......………… la tarehe ……….........…………

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu chaa 7(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA ZA MWAKA 2018

Jina la sheria ndogo hizi **1** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018* na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi **2** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Tafsiri **3** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo;-

"Ada" maana yake ni tozo, kodi, ushuru au malipo yatakayolipwa na mtu yeyote kwa Halmashauri kwa ajili ya kupata kibali, huduma ya leseni, ukaguzi wa ramani na majengo, ukaguzi wa viwanja, upimaji wa viwanja, uhamishaji miliki ya viwanja, uchapishaji stakabadhi, zabuni, kodi ya pango, adhabu za makosa ya barabarani yanayokusanywa na traffic, adhabu zitokanazo na makosa mbalimbali zinazoamuriwa na Mahakama za chunya na huduma nyinginezo.

"Afisa Masuuli" maana yake ni Mkurugenzi au Afisa yeyote atakayeidhinishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Mwanasheria wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri au Mkurugenzi kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

"Barabara" maana yake ni barabara zote zilizo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri zinazo milikiwa na kuhudumiwa na Halmashauri, TARULA au Serikali Kuu.

“Biashara” maana yake ni uendeshaji wa shughuli yoyote halali inayomuingizia mtu kipato.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

“Jengo” maana yake ni jengo lolote la makazi au biashara, kiwanda, lililojengwa kwa kutumia vifaa vya aina yoyote ile na ni pamoja na jengo liliojengwa kwa kutumia udongo, nyasi na miti, jengo la biashara, makazi, kibanda, kontena, turubai, mwavuli uliosimikwa kwa ajili ya shughuli za biashara katika eneo lolote ambalo limeruhusiwa kutumiwa na mtu kibiashara katika eneo la mamlaka ya Halmashauri.

“Kibali” maana yake ni kibali chochote cha maandishi kilichotolewa na Mkurugenzi au Afisa Mwindhiniwa kwa mtu yeyote anayepata huduma yoyote au mtu anayepata huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

“Kibanda” maana yake ni kibanda chochote cha biashara kilichojegwa katika eneo linalomikiwa na Halmashauri au mtu binafsi.

“Kodi ya pango” maana yake ni kodi ya pango itakayolipwa na mtu yeyote aliyepanga katika kibanda cha biashara, meza za soko, eneo au jengo lolote la Halmashauri pamoja na vibanda vya biashara vilivyojengwa na watu binafsi katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri.

“Machinjio” maana yake ni machinjio yanayo milikiwa na Halmashauri au sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuchinja wanyama au kuanikia ngozi za wanyama waliochinjwa.

“Madini” maana yake ni dhahabu, shaba galena, copper, chuma, mawe, kokoto, mchanga wa ujenzi, udongo wa aina yoyote au mali yoyote ipatikanayo aridhini chini ya sheria ya madini.

“Malori” maana yake ni magari yote ya mizigo isipokuwa

landlover au pick up.

“Mazao” au “zao” maana yake ni mazao ya kilimo ufuta, mahindi, mtama, korosho, alizeti, tumbaku, pamba, karanga, ngano, viazi maharage, nyanya, vitunguu, njegele, kunde, dengu, njugu, mazao ya misitu, asali, inajumuisha pamoja na nafaka na matunda aina za ndizi mbivu, ndizi za kupika, miwa, matunda aina ya nanasi, machungwa, parachichi, tikiti-maji, maembe na mazao mengine yanayopatikana chunya.

“Mazao ya misitu” maana yake ni mbao, magogo, mkaa, kuni, asali, nta na mazao mengine yatokanayo na misitu

“Mfanyabiashara” maana yake ni mfanyabiashara yeyote anayeuza bidhaa katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na mfanyabiashara Ndogondogo au machinga.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakaye kuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi ikiwa pamoja na Mwanasheria wa Halmashauri kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

“Mtu” maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, taasisi au kampuni ambayo inafanya biashara ya aina yoyote katika eneo la Halmashauri,

“Soko” maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri ya Wilaya au kijiji kama soko kwa ajili ya huduma ya umma.

“Stakabadhi” maana yake ni stakabadhi ya kieletroniki au stakabadhi nyingine iliyoruhusiwa na serikali itakayotolewa na Halmashauri kama uthibitisho wa malipo ya ada au ushuru.

“Stendi” maana yake ni eneo lolote la kiyuo cha magari, pikipiki, bajaji au guta.

"Takataka" maana yake ni taka ngumu, taka maji au kimiminika pamoja na taka laini.

"Ushuru" maana yake ni tozo ya huduma mbalimbali au tozo ya biashara mbalimbali za kawaida au kiwanda.

"Wakala" maana yake ni taasisi au kampuni au mtu binafsi aliyeteuliwa au kuingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru au ada kwa niaba ya Halmashauri.

Ada na Ushuru

**4** (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika biashara, huduma mbalimbali, adhabu zitokanazo na makosa ya barabarani (trafic offence), adhabu zilizohukumiwa na kuamriwa na Mahakama za Chunya, ada za vyeti vya ndoa, ada za vyeti vya kifo, ada za pango za majengo mbalimbali, ada za matangazo, ada za umiliki wa vitalu vya madini, ada za umiliki wa silaha, ada za ardhi, ushuru wa mazao mbalimbali, ushuru wa minada, ada za vibali au leseni mbalimbali, kama ilivyoorodheshwa katika majedwali yaliyopo katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mtu au taasisi itakuwa na wajibu wa kulipa ushuru au ada kwa kuzingatia viwango vya sheria hii.(Jedwali la ada na ushuru)

Ushuru unaohusu mifugo

**5** (1) Halmashauri itatoza ushuru wa mifugo kwa ajili ya machinjio kwa kila mnyama atakayechinjwa katika machinjio ya Halmashauri na ushuru wa mnada wa mifugo kwa mifugo itakayouzwa mnadani kwa kiwango kilichoidhinishwa kwenye Sehemu A Jedwali I la Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote

(a) Kuchinja ng'ombe, mbuzi, kondoo au nguruwe nje ya eneo lililotengwa au kuindhinishwa na Halmashauri kama eneo la machinjio.

(b) Kuuza nyama ambayo haikupimwa au haikukaguliwa na mtalamu wa mifugo.

(c) Kuuza mifugo nje ya maeneo yaliyoruhusiwa au nje yam nada wa mifugo.

Ushuru wa madini.

**6** (1) Halmashauri itatoza ushuru wa madini yaliyopatikana ndani ya eneo la Halmashauri kwa kiwango kilichoidhinishwa kwenye Sehemu B Jedwali I la Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) Kuchimba madini katika eneo lisiloruhusiwa na Ofisi ya madini au Halmashauri.

(b) Kuchimba, kusafirisha madini bila kuwa na kibali cha kutoka mamlaka ya madini au Halmashauri.

Ushuru wa Stendi.

**7** (1) Halmashauri itatoza ushuru kwa magari yanayoingia na kutoka nje ya kituo cha stendi kwa kiwango kilichoidhinishwa kwenye Sehemu C Jedwali I la Sheria Ndogo hizi.

(2) Magari yafuatayo hayatatozwa ushuru wa stendi.

i) Magari ya serikali na wanaadiplomasia.

ii) Magari ya majeshi yote ya ulinzi na usalama na polisi

iii) Magari ya wagonjwa na ya usafi.

Ada za kukodi na kupanga.

**8** (1) Halmashauri itakodisha mali, mitambo, magari, kumbi na itapangisha, nyumba za kuishi na vizimba au vibanda vinavyomilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanyia biashara kwa kiwango kilichoidhinishwa kwenye Sehemu D Jedwali I lililopo kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayehitaji kukodi au kupangishwa mali yoyote, nyumba, kibanda, vizimba, gari au ukumbi na Halmashauri atapaswa kuwasilisha maombi yake kwa Afisa Masuuli ambapo iwapo atakubaliwa atapaswa kuingia Mkataba na Halmashauri wa ukodishaji au upangaji.

Ada za kibali cha ujenzi na huduma nyingine za ardhi

**9** (1) Halmashauri itatoza ada za kibali cha ujenzi na huduma nyingine za ardhi kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sehemu E Jedwali I la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali cha ujenzi kitatolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri baada ya kuidhinishwa na kamati Ndogo ya mipango miji, Afya na mazingira na ujenzi.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga jengo bila kupewa kibali cha ujenzi na Halmashauri.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mamlaka na uwezo wa Halmashauri | **10** | | Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupanga muda maalumu wa kufungua/kufunga soko na kuamuru kufunga biashara yoyote ya mmiliki au mtumiaji wa huduma yoyote endapo mmiliki au mtumiaji atakataa kulipa ada, ushuru au kibali kama ilivyoorodheshwa chini ya Sheria Ndogo hizi. |
| Namna ya kukusanya Ada na Ushuru | **11** | (1) | Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona unafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru katika vyanzo vya mapato mbalimbali. |
| | | (2) | Malipo ya Ada au Ushuru yatakayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielekroniki au nyingine iliyoruhusiwa na serikali kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika. |
| | | (3) | Malipo yatathibitishwa kwa kuonyesha stakabadhi ya Halmashauri na hautakuwa utetezi kwa mmiliki au mtumiaji kudai kwamba amelipa na hakupewa stakabadhi. |
| | | (4) | Ada au Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali au kwa kuzingatia utaratibu mwingine utakaotolewa na Mkurugenzi. |
| | | (5) | Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au wakala kwa idhini ya Afisa Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika endapo stakabadhi ya kieletroniki haiwezi kutolewa. |
| Utaratibu wa kukusanya madeni ya ada na ushuru | **12** | (1) | Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yoyote endapo ameshindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Endapo bidhaa au mali itakayokamtwa na Halmashauri au wakala haitolipiwa Ada au Ushuru unaodaiwa ndani ya siku kumi na nne kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa kwa mali zinazoharibika haraka, Halmashauri itakua na mamlaka ya kuuza bidhaa au mali na fedha |

zitakazopatikana zitawekwa kwenye akaunti ya Halmshauri.

(3) Wakala hataruhusiwa kuuza bidhaa iliyokamatwa chini ya fungu la 2 la kifungu cha 12 cha Sheria Ndogo hizi bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

(4) Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada na ushuru kwa njia ya mahakama, kwa kuwakamata watu wote waliokataa kulipa ada na ushuru na kuwashitaki kwa jinai Mahakamani.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa hasara itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zilizokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.

Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru

**13** (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu wa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

Ada na ushuru wa umiliki wa silaha

**14** (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kutoza ada na ushuru kwa kila mmiliki wa silaha anayetambulika na kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Chunya.

(2) Ada na ushuru wa kila silaha itakuwa shilingi elfu ishirini kwa kila mwaka kwa kila silaha.

Ada na ushuru(vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya ndoa

**15** (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupata kiasi cha fedha itokanayo na tozo za vyeti vya ndoa na vyeti vya kuzaliwa.

(2) Mamlaka zinazotoa vyeti vya kuzaliwa, na vyeti ndoa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya zitaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba asilimia tano 5% ya gharama ya cheti zitakuwa zinakatwa kama ada na ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Ada na ushuru za

**16** (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupata kiasi cha fedha asilimia 5% faini za makosa barabarani (traffic offences) yanayotozwa na

| | | | |
|---|---|---|---|
| makosa ya barabarni(traffic offences) | | (2) | askari wa usalama barabarani<br><br>Mkuu wa Polisi Wilaya ya Chunya au Mkuu wa usalama barabarani (Traffic) atahakikisha kiasi cha fedha za adhabu ya faini za makosa barabarani 5% kinatunzwa kwa ajili Halmashauri. |
| Mapato yatokanayo na hukumu za faini za Mahakamani | **17** | (1) | Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupata kiasi cha fedha asilimia 5% itokanayo na faini za makosa mbalimbali ynayohukumiwa kwenye Mahakama za Chunya. |
| | | (2) | Hakimu Mfawidhi au Mtendaji wa Mahakama ataweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba asilimia tano 5% ya faini zilizohukumiwa au kuamriwa Mahakamani zitakuwa zinakatwa kama ada na ushuru wa huduma kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. |
| Uteuzi wa wakala | **18** | | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteuwa mtu, Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi |
| Wajibu wa wakala | **19** | | Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa na wajibu wa:- |
| | | (a) | Kukusanya na kupokea Ada au Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (b) | Wakala atakusanya Ada au Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri. |
| Makosa kwa wakala | **20** | | Itakuwa ni kosa kwa wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:- |
| | | (1) | Atajaribu au atakusanya Ada au Ushuru bila idhini ya Halmashauri. |
| | | (2) | Atajaribu au atakusanya Ada au Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi. |
| | | (3) | Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada au Ushuru kilichokubaliwa katika mkataba wa kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | (4) | Atashindwa kutoa stakabadhi halali ya malipo kwa Ada au Ushuru |

aliokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(5) Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja na kulipa kiasi cha fedha anachodaiwa.

Ada ya kufungua shauri kwenye mabaraza ya kata

**21** (1) Isipokuwa mashauri ya jinai, kila shauri la madai au kesi ya madai inayofunguliwa kwenye baraza la kata italipiwa ada ya kufungua shauri shilingi elfu thelathini.

(2) Ada italipwa kwa katibu wa baraza la kata husika wakati mdai anafungua shauri kwenye baraza hilo.

Makosa

**22** Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-

(1) Atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashuri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataaa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(3) Atamzuia kwa namna yoyote ile Mwanasheria Halmashauri au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri au atafanya biashara ya mazao bila kibali.

(5) Atashindwa/ Atakataa kutoa taarifa za hesabu zake za biashara au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(6) Atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru na kusingizia kukwepa kulipa au atakayekataa gari lake lisikaguliwe getini au kizuizi chochote

Adhabu

**23** (1) Mtu yoyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi

kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri faini ya shilingi laki tatu, gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza.

Kufifilisha kosa **24** Mkurugenzi Mtendaji, Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi au Mwanasheria wa Halmashauri watakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki tatu (300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la II la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa sheria ndogo **25** Sheria ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2015 zilizotolewa kwenye Tangazo la serikali namba 485 la tarehe 30/10/2015 ZIMEFUTWA .

JEDWALI NA. I
SEHEMU A
Limetungwa chini ya kifungu cha 5(1) cha sheria ndogo hizi

1. USHURU WA MACHINJIO

| Na | Mnyama | Kiasi (Tshs) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2000/= | Kila ng'ombe mmoja |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 1000/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |
| 3. | Nguruwe | 1000/= | Kila nguruwe mmoja |

2. USHURU WA MIFUGO INAYOUZWA KWENYE MAENEO YA MNADA

| Na | Mfugo | Kiasi (Tshs) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | 6000/= | Kila ng’ombe mmoja |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 3000/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |
| 3. | Nguruwe | 2000/= | Kila nguruwe mmoja |
| 4. | Kuku | 500/= | Kila kuku |

3. USHURU WA NGOZI

| Na | Aina ya ngozi | Kiasi(Tsh) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ngozi ya ng’ombe | 500/= | Kwa kipande |
| 2. | Ngozi ya mbuzi au kondoo | 200/= | Kwa kipande |

4. ADA NA USHURU WA HUDUMA NYINGINE KWA AJILI YA MIFUGO

| Na | Aina ya mfugo | Kiasi(Tsh) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kusajili/kutoa kadi ya mfugo au kupiga chapa (Ng’ombe) | 2000/= | Kwa kila ng’ombe |
| 2. | Kusajili mbuzi au kondoo au chapa | 1000/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Kusajili au kupiga chapa (Punda) | 1500/= | Kwa kila mnyama |
| 4. | Chanjo ya mifugo Ng’ombe | 500/= | Kwa kila mfugo utakaochanjwa |

SEHEMU B

Chini ya kifungu cha 6 cha sheria ndogo hizi

ADA NA USHURU UTOKANAO NA UCHIMBAJI NA UCHENJUAJI WA MADINI

1. ADA NA USHURU UTOKANAO NA MADINI YA DHAHABU

| Na | Mtambo/Shughuli/Chanzo | Kiasi (Tshs) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya umiliki wa kitalu cha madini (PML) | 30,000/= | Kila kila kitalu kwa mwaka |
| 2. | Plant ya kuchenjua | 1,000,000/= | Kila planti kwa mwaka |
| 3. | karasha | 100,000/= | Kila karasha kwa mwaka |
| 4. | Elution | 1,000,000/= | Kila elution kwa mwaka |
| 5. | Ada/Leseni ya Mnunuzi | 1,000,000/= | Kila mnunnuzi wa madini kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa madini (Digala) | | mwaka |

2. ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI MCHANGA, KOKOTO, MAWE

| Na | Ukubwa wa gari | Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Gari tani 1 | 1000/= Kwa Safari |
| 2 | Gari tani 2 | 2000/= Kwa Safari |
| 3 | Gari tani 3 | 2500/= Kwa Safari |
| 4 | Gari tani 4-6 | 3000/= Kwa Safari |
| 5 | Gari tani 7 | 5000/= Kwa Safari |
| 6 | Gari tani 8 na kuendelea | 8,000/= Kwa Safari |
| 7 | Usafirishaji wa vifaa vingine vya ujenzi kama matofali Ushuru utatozwa kwa mchanganuo kama ulivyotolewa hapo juu. | |

SEHEMU C

Chini ya kifungu cha 7

USHURU WA STENDI NA VITUO VINGINE VITAKAVYOANZISHWA NDANI YA HALMASHAURI KWA AJILI YA VYOMBO VYA MOTO

| Na | Aina ya Vyombo/gari | Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Basi la abiria zaidi ya 40 | 2500/= Kila linapotoka kituoni |
| 2 | Basi abiria 20 – 40 | 2000/= Kila linapotoka kituoni |
| 3 | Basi la abiria 1 – 20 | 1500/= Kila inapotoka kituoni |
| 4 | Taxi | 1000/= Kila inapotoka kituoni |
| 5 | Magari mengine yasiyo ya biashara | 1000/= Kila inapotoka kituoni |

SEHEMU D

Chini ya kifungu cha 8

ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na | Aina ya mali | Ada |
|---|---|---|
| 1 | Kukodisha ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya semina au shughuli binafsi | 600,000/= Kwa siku (masaa ya kutumia hayatazidi 8 kwa siku) |
| 2 | (a) Kupanga kizimba cha biashara sokoni | 4,000/= Kwa mwezi |
| | (b) Kupanga chumba au kibanda eneo la kituo cha mabasi (stendi). | 25,000/= Kwa mwezi kwa kila chumba |

| | | |
|---|---|---|
| | (c) Kupanga chumba kuzunguka soko la uhindini | 15,000/= Kwa mwezi |
| | (d) Kupanga chumba cha ndani soko la uhindini au soko kuu | 15,000/= Kwa mwezi |
| 3 | Kukodi magari madogo | 2000/= Kwa kilometa moja |
| 4 | Kukodi magari makubwa | 3500/= Kwa kilometa moja |
| 5 | Kukodi pikipiki | 20,000/= Kwa masaa nane |
| 6 | Kukodi mashine nyingine yoyote | 500,000/= Kwa kila masaa kumi |
| 7 | Kodi ya viti na meza za Halmashauri | 500/= Kwa mkataba |
| 9 | Kukodi ardhi kwa matumizi maalum | Kwa mkataba |

SEHEMU E

Chini ya kifungu cha 9

ADA ZA HUDUMA ZA ARDHI

| Na | Kibali cha ujenzi | | Kiasi(Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ghorofa zaidi ya kuendelea | | 300,000/= |
| 2. | Taasisi mbalimbali | | 250,000/= |
| 3. | Ghala au bohari | | 200,000/= |
| 4 | Kituo cha Mafuta, Hoteli | | 250,000/= |
| 5 | Viwanda vya huduma (Service Industrial Plot) | | 150,000/= |
| 6 | Nyumba za makazi | | 100,000/= |
| 7 | Nyumba za makazi na biashara | | 200,000/= |
| 8 | Ramani ya kitalu (Block Plan) | | 50,000/= |
| 9 | Ghorofa 1 (Multi Storey Structures) | | 300,000/= |
| 10 | Mnara | | 2,500,000/= |
| 11 | Majengo mengine yote ambayo hayakutajwa | | 200,000/= |
| 12 | Viwanda (Industrial Plot) | | 250,000/= |
| 13 | Uzio wa matofali (fence) | | 50,000/= |
| 14 | Kibali kidogo cha ukarabati wa jengo | | 50,000/= |
| | **Ada na Vibali vya kujenga, kubadilisha matumizi ya Ardhi, kugawa viwanja,mashamba na au kurekebisha mchoro** | | |
| | Matumizi ya Awali | Matumizi yanayoombwa | Kiasi(Tsh) |
| 1 | Makazi pekee | Makazi na biashara | 100,000/= |
| 2 | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja | 100,000/= |
| 3 | Makazi pekee | Shule ,Hosteli,Zahanati na huduma nyinginezo za jamii | 150,000/= |
| 4 | Makazi pekee | Hoteli | 200,000/= |
| 5 | Makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 200,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Makazi na biashara | (Maduka makubwa ) Super Market/Shooping Mall | 200,000/= |
| 7 | Makazi pekee | (Viwanda/huduma) Service Trade/Industrial | 200,000/= |
| 8 | Makazi pekee | Ghala (Yard/Godown) | 200,000/= |
| 9 | Biashara | Makazi | 100,000/= |
| 10 | Kugawa shamba kuwa viwanja vya makazi | makazi | 100,000/= |
| 11 | Kugawa kiwanja cha makazi | makazi | 100,000/= |
| 12 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya hoteli | biashara | 200,000/= |
| 13 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya shule, hosteli, zahanati na huduma nyinginezo za jamii. | biashara | 100,000/= |
| 14 | Ada ya uhakiki wa umiliki kiwanja au shamba (Official Search) | Matumizi yoyote | 50,000/= |
| 15 | Ada ya maombi ya kununua kiwanja | Matumizi yoyote | 20,000/= |

SEHEMU F

ADA NA LESENI ZA KIBALI NA USHURU MWINGINE

Chini ya sheria ndogo hizi

| Na | Aina ya ada/Kibali au Ushuru | Kiasi(Tsh) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya utambulisho(stika za Halmashauri) kwa ajili ya vyombo vya huduma ya usafiri bodaboda, bajaji, guta, tax, na daladala | 10,000/= kwa kila stika (itadumu kwa mwaka mmoja) |
| 2. | Umiliki wa silaha | 20,000/= kwa mwaka kila silaha |
| 3. | Ada ya kufungua kesi ya madai kwenye baraza la kata | 30,000/= kila shauri/kesi itakayofunguliwa |
| 4. | Ada ya maombi ya nakala ya hukumu kwenye kesi za madai kwenye baraza la kata | 10,000/= kwa kila shauri litakalotolewa hukumu. |
| 5. | Ada zitokanazo na adhabu za makosa mbalimbali barabarani (Trafic offence) | 5% ya jumla ya faini ya adhabu itakayotolewa kwa kila kosa |
| 6. | Ada zitokanazo na adhabu za makosa mbalimbali | 5% ya jumla ya faini ya |

| | | |
|---|---|---|
| | kwenye Mahakama za Chunya | adhabu itakayotolewa |
| 7. | Ada na leseni au kibali cha kununua mazao | 100,000/= kwa kila kibali na kitadumu kwa mwaka mmoja. |
| 8. | Ushuru wa mazao ya biashara | 3% ya bei ya soko |
| 9. | Ushuru wa mazao ya misitu | 3% ya bei ya soko |
| 10. | Ushuru wa Ada ya mazao ya chakula | 2% ya bei ya soko |
| 11. | Ada na ushuru wa nyumba binafsi zilizopangishwa | 5% ya bei ya pango |
| 12. | Ada ya maombi ya cheti cha ndoa/ cheti cha kuzaliwa | 5% ya jumla malipo ya cheti |
| 13. | Ushuru wa pango la mnara wa simu kama kiwanja cha ni cha mtu binafsi | Shilingi 100,000/= kwa mwaka (utalipwa na miliki wa kiwanja au mmiliki wa mnara |
| 14. | Ada na ushuru wa vibanda vya huduma za fedha kupitia simu za mkononi | 80,000/= kwa mwaka |
| 15. | Ada na leseni ya cha night club | 300,000/= kwa mwaka |
| 16. | Ada na leseni ya kumbi za vikao na starehe zingine | 100,000/=kwa mwaka |
| 17. | Ada ya maombi ya kibali cha mziki | 700,000/= kwa siku |
| 18. | Ada ya maombi ya kibali cha tangazo la biashara | 100,000/= kwa masaa nane |
| 19. | Ada ya kibali cha mambo mengine ya kiutamaduni | 100,000/= kwa mwaka |
| 20. | Ada ya maombi ya kibali cha tangazo la sherehe | 50,000/= kwa siku |
| 21. | Ada ya kusajili timu ya mchezo | 80,000/= kwa kila uasajili |
| 22. | Ada ya kibali cha mchezo wa magari au pikipiki | 100,000/= kwa masaa sita |
| 23. | Ada ya usafi na uzoaji taka majumbani(maeneo ya mji) | 1000/= kwa mwezi |
| 24. | Ada ya usafi na uzoaji taka ofisini/ biashara (maeneo ya miji) | 10,000/= kwa mwezi |
| 25. | Ada ya kibali cha kutembeza bidhaa | 30,000/=kila kibali |
| 26. | Ada ya maombi ya kusafirisha kemikali zozote | 100,000/= |
| 27. | Ada na ushuru wapombe za kienyeji | 2000/= kwa pipa |
| 28. | Ada ya maombi ya kuweka bango barabarani | 50,000 kwa kila bango |

JEDWALI II
(Limetungwa chini ya kifungu cha 24)

KUFIFILISHA KOSA

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya………………………………………ambaye ni Mkurugenzi, au Mtendaji wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi au Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwamba mnamo

tarehe……ya mwezi……………..mwaka ………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018. (Ambapo najutia kosa langu na kukiri kutorudia tena)

Kwahiyo kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri au Mwanasheria niko tayari kulipa kiasi cha Ada ya kibali/leseni au Ushuru ninaodaiwa shilingi……………………….. pamoja na faini ya shilingi…………………………au jumla shilingi……………………………..
Kiasi hicho kitalipwa siku ya tarehe……………………………… bila kukosa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YA HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU NA SIJALAZIMISHWA NA MTU.
Leo tarehe…………………ya mwezi…………………Mwaka…………Nikiwa eneo la………...
Saini……………………………Majina…………………………………Simu…………………
Kijiji/Kitongoji ninachoishi……………………………………Kata………………………………

Mbele ya:

Saini………………………………………..
Jina…………………………………………
Wadhifa………………………………………

TANGAZO LA SERIKALI Na …......…………. la tarehe ………..

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA KUSIMAMIA MAENDELEO NA VIWANDA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA ZA MWAKA, 2018

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kuanza kutumika | **29.** | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo za (Ushiriki wa Wananchi kusimamia Maendeleo na Viwanda) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018* na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |

Matumizi **30.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Tafsiri **31.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

**"**Afisa Mwidhiniwa**"** maana yake ni Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

**"**Afisa Mtendaji**"** maana yake ni Afisa wa kata au kijiji aliyeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi za Afisa Mtendaji kwenye eneo la kata ama kijiji.

**"**Baraza la kata" maana yake ni Baraza la kata lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata.(Ward Tribunal)

**"**Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Halmashauri za Vijiji vya Wilaya ya Chunya.

**"**Kazi**"** maana yake ni shughuli yoyote ile ambayo ni halali inayoweza kumuingizi mtu kipato.

**"**Kiongozi wa eneo**"** maana yake ni Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji/Kata, Diwani wa Kata, Afisa Tarafa, Mkuu wa Kituo cha Polisi, Mkurugenzi Mtendaji, Hakimu, Mbunge na Mkuu wa Wilaya.

**"**Kushiriki maendeleo" maana yake ni kushiriki katika kazi zote za maendeleo ya umma kupitia nguvu kazi au michango inayoamriwa kwenye mikutano ya vitongoji, vijiji au Vikao vya maendeleo vya kata na Baraza la Madiwani.

**"**Kupinga maendeleo" maana yake ni mtu kukataa kushiriki kufanya kazi/shughuli za pamoja au kukataa kutoa mchango ulioamriwa na mikutano ya vijiji au vikao vya maendeleo vya kata kwa ajili ya maendeleo.

**"**Kiwanda**"** maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye sheria ya viwanda na kwenye sera ya nchi kuhusu maendeleo ya viwanda ikiwa ni pamoja na uwekezaji.

**"**Kushiriki maendeleo" maana yake ni kushiriki kwenye kazi zote za pamoja za umma kwa kutoa nguvu kazi au mchango wa fedha au mali nyingine ili iendeleze kujenga shule, ofisi yoyote ya serikali, zahanati/kituo cha afya au barabara

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi ikiwa ni pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi.

"Mtendaji Mkuu" maana yake ni mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi.

"Mazao" maana yake ni mazao yanayolimwa kwa ajili ya chakula, asali, mazao yanayolimwa kwa ajili ya biashara, na mazao yatokanayo na mali asili kama vile mbao na mazao mengine.

"Madini" maana yake ni dhahabu, copper, galena zink, Makaa ya mawe, Alumasi, kokoto na Mchanga.

"Mkazi" maana yake ni mtu anayetambulika kuwa ni mkaaji wa eneo la kitongoji, au kijiji na mwenye makazi yoyote ya kujenga mwenyewe au kupanga.

"Makazi holela" maana yake ni makazi yaliyoanzishwa bila kufuata taratibu zilizowekwa na Afisa Mipango miji au Serikali ya Kijiji.

"Maendeleo" maana yake ni mambo yote ya pamoja ya umma ikiwa ni pamoja na shule, zahanati, vituo vya afya, barabara, ofisi za serikali kuweka miundombini mizuri ya maeneo ya maziko.

"Magonjwa ya mlipuko" maana yake ni kipindupindu na magonjwa mengine yanayoibuka ghafla na yanauewzo wa kumdhuru binadamu, mifugo na mimea.

"Masaa ya kuruhusiwa kunywa pombe" maana yake ni muda maalumu wa kunywa pombe aina zote siku za kuanzia jumatatu hadi ijumaa itakuwa kuanzia saa tisa jioni hadi saa tano usiku kila siku na siku za jumamosi na jumapili itakuwa kuanzia saa sita mchana hadi saa sita usiku vinginevyo mtu atakuwa ametenda kosa la kuvunja sheria ndogo hii.

"Michango" maana yake ni mtu kutoa fedha, mali au nguvu kazi kwa ajili ya kuendeleza maendeleo.

“Mwanasheria” maana yake ni mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

“Ushiriki wa wananchi” maana yake ni wananchi kushiriki kupitisha miradi ya maendeleo na kuchangia fedha au nguvukazi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo ya umma.

“Uzurulaji” maana yake ni kitendo cha mtu mwenye uewzo wa kufanya kazi lakini wakati wa masaa ya kufanya kazi anakaa na wenzake vijiweni kwa kupiga soga, kucheza bao, karata, drafti au mchezo wowote badala ya kufanya kazi.

“Uwekezaji” maana yake ni kuanzisha kiwanda chochote, kufungua elution au mgodi wa kuchimba au kuzalisha madini au namna nyingine yoyote ya uwekezaji

“Viwanda”maana yake ni tawi la kampuni lililosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.

“Shughuli za maendeleo” maana yake ni kazi zote za jamii za kuanzisha au kuendeleza barabara, miradi ya maji, shule vituo vya afya vituo vya polisi, Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo, ujenzi wa ofisi za kijiji/kata au shughuli za mradi wowote zitakazoafikiwa na mikutano ya vijiji au vikao vya vya maendeleo vya kata au Halmashauri ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye siku maalumu ya shughuli za usafi wa mazingira.

Wananchi kushiriki shughuli za maendeleo

**32**. Itakuwa ni wajibu wa kila Mwananchi mwenye umri wa kuanzia miaka kumi na nane ambaye hajasajiliwa na kutambulika kama mwanafunzi wa shule ya Sekondari au Chuo chochote atashiriki kwenye shughuli za maendeleo.

Mpango wa shughuli za maendeleo

**33**. (1) Wananchi kwenye kila kitongoji wanaweza kuamua na kuweka mpango wa shughuli za maendeleoa kwenye eneo lao.

(2) Wananchi kupitia Mkutano wa Kijiji wanaweza kuamua na kuweka mpango na utaratibu wa shughuli za maendeleo ya eneo lake.

(3) Kamati ya maendeleo ya kata inaweza kupendekeza mpango wa maendeleo ya eneo lake na kupeleka hoja ipitishwe na Mkutano wa kijiji kwa ajili ya utekelezaji.

Michango ya maendeleo

**34**. (1) Kila mwananchi Mkazi atalazimika kushiriki kuchangia maendeleo kwa:-

a) Kutoa mchango wa nguvu kazi ama mali yoyote au

b) Kutoa mchango wa fedha kwa kiwango kilichoruhusiwa au kutoa zaidi.

(2) Michango yote ya maendeleo itahamasishwa na viongozi na michango itakusanywa na Watendaji au mtu yeyeto aliyeruhusiwa na viongozi au kuteuliwa na Mkutano kufanya kazi ya kukusanya michango.

Udhibiti unywaji wa pombe na kucheza pool muda wa kazi

**35.** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo atakuwa:-

a) Anakunywa pombe muda usioruhusiwa kisheria.

b) Anacheza pool table muda wa masaa ya kazi au muda usioruhusiwa kisheria

(2) Iwapo mtu atakutwa anakunwa pombe, anacheza pool table muda usioruhusiwa akipatikana atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kushitakiwa kwenye Baraza la kata au Mahakama ya Mwanzo/Wilaya na kulipa faini kuanzia laki moja hadi laki tatu au kuhukumiwa kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Daftari la rejesta ya maendeleo ya wakazi

**36.** Kila mkazi wa eneo la kitongoji au kijiji atatakiwa kujiandikisha kwenye daftari la maendeleo ya wakazi. Orodha hiyo itakuwa na

(a) Majina kamili ya mkazi na familia yake pamoja na umri wa watoto kama wapo

(b) Kazi za kila siku za kuingiza kipato anazofanya kila Mkazi na mahalli anakofanyia kazi

(c) Jina la Mtaa au kitongoji anachoishi. Je ana makazi yake aliyojenga, kama ni mpangaji jina la mmiliki wa nyumba.

(d) Mkataba wa pango utaambatanishwa kwa wale wanaoishi nyumba za kupanga.

Viwanda na uwekezaji

**37.** Itakuwa ni jukumu la kila kijiji kuweka mpango wa kuanzisha fursa ya kufungua viwanda na uwekezaji kwa kutenga ardhi na maeneo ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Taratibu za uwekezaji wa viwanda

**38**. (1) Uwekezaji wa viwanda utafuata taratibu zifuatazo:-

d) Mwekezaji kuonyesha vibali na leseni ya uwekezaji kutoka mamlaka inayohusika

e) Mwekezaji kutambulika na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu uwekezaji baada ya kukata leseni ya Halmashauri.

f) Mwekezaji kuonesha mkataba wake wa ardhi iwapo umetokana au amepata kwa mtu binafsi

g) Mwekezaji kujadiliwa na kupitishwa na mkutano Mkuu wa Kijiji na Muhtasri kufikishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji

(2) h) Mwekezaji kuingia na kusaini Mkataba kati yake na kijiji husika juu ya namna atakavyochangia huduma za jamii. Mkataba huo lazima uthibitishwe na Mwanasheria wa Halmashauri.

(3) Taratibu za uwekezaji wa viwanda zinazoelezewa kwenye kifungu hiki cha 10 cha sheria ndogo hizi itakuwa ni pamoja na kufungua mtambo/mnara wa simu, elution ya kuchenjua madini, kuanzisha mgodi wa kuchimba madini au namna nyingine yoyote inayohusu uwekezaji.

Mtu yeyote anayeamua na kuomba kuwekeza kwenye eneo lolote la Halmashauri atatakiwa kufuata taratibu zote na kuridhia kulipa ada na kodi zote za serikali.

Udhibiti wa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji

**39**. (1) Eneo lolote la ardhi lililomriwa kwa ajili ya uwekezaji litakuwa kwa ajili ya matumizi hayo tu.

(2) Mtu yeyote atakayebadilisha matumizi ya eneo la uwekezaji akalitumia kwa shughuli nyingine atakuwa amepoteza sifa ya kuwa mwekezaji na eneo lake litanyang'anywa na kuwa mikononi mwa serikali.

Uendeshaji wa viwanda na uwekezaji mwingine

**40**. (1) Mmiliki wa kiwanda atahakikisha kwamba shughuli zote zisizohusu utaalamu zinakuwa ani ajira ya Wananchi wa Wilaya ya Chunya.

(2) Vingozi wote waliotajwa kwenye sheria hii wataweka utaratibu maalumu wa kukagua taratibu za uendeshwaji wa kiwanda na uwekezaji.

Makosa **41**. (1) Mtu yeyote yule atakuwa ametenda kosa iwapo bila sababu za msingi:-

(s) Atakataa au kushindwa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo bila sababu za msingi.

(t) Atakataa kuorodheshwa kwenye daftari la maendeleo

(u) Atakataa kutoa mchango halali wa maendeleo.

(v) Atavamia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji.

(w) Akifanya shughuli za uwekezaji wa kiwanda bila kufuata taratibu

(x) Akinywa pombe masaa yasiyoruhusiwa kisheria.

(y) Akiwa anacheza pool table masaa yasiyoruhusiwa.

(z) Akiwa anafanya uzurulaji wa aina yoyote

(aa) Akikaidi kusitisha shughuli zake baada ya kutolewa ilani ya magonjwa ya mlipuko

(bb) Akiharibu miundombinu ya yoyote.

(cc) Atamzuia au atajaribu kumzuia afisa muidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu **42**. (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza.

Kufifilisha kosa **15** Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mmlaka ya Mji mdogo wa Makongolosi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki tatu (300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la I la Sheria Ndogo hizi na

atatakiwa kulipa gharama zingine za ukamataji.

## JEDWALI LA I

## KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa Chini ya kifungu cha 15

Mimi…………………………………………….nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya……………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, kwamba mnamo tarehe……………………………………………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ushiriki wa Wananchi katika kusimamia maendeleo na Viwanda) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018.

Nakiri kwamba nimetenda kosa na niko tayari kulipa faini na gharama zingine kiasi cha jumla shilingi…………………………………………………………………………………………

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YOTE NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU NA SIJASHINIKIZWA NA MTU YEYOTE.

Maelezo yametolewa leo tarehe…………………………………………………..……….

Saini yangu………………………………………………..Simu yangu………………….

Majina yangu…………………………………………………………………………

Mbele ya:

Saini yake……………………………………………………....

Majina yake………………………………………………………….

Cheo Chake………………………………………………………….

Simu yake………………………………………

TANGAZO LA SERIKALI NA. ………… la tarehe …………………..

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO YA (HIFADHI YA ARDHI, MAZINGIRA NA UCHIMBAJI WA MADINI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA, 2018

**SEHEMU YA I**
**MAELEZO YA AWALI**

*Jina na tarehe ya kuanza kutumika*

**1.** -Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama *Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Ardhi Mazingira na Uchimbaji wa Madini) ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2018* na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

*Matumizi*

**2.** -Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

*Tafsiri*

**3.** -Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa tu kama itaelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Afya" maana yake ni Afisa wa Afya aliyeajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

"Afisa Mazingira" maana yake ni mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya anayeshauri, kusimamia na kuratibu masuala yote ya mazingira katika mamlaka ya Halmashauri;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri ya Jiji la Arusha anayesimamia sheria ndogo hizi;

"Ardhi hatarishi" maana yake ni ardhi ambayo ikiendelezwa inaweza kuleta hatari katika maisha au kusababisha uharibifu wa mazingira katika ardhi hiyo au nyingine inayopakana nayo.

"Ardhi Oevu" maana yake maeneo yote ya ardhi ambayo ni vyanzo vya maji.

"Chukizo" maana yake ni kero au kitu chochote kinachoweza kuleta madhara au kuhatarisha afya ya binadamu;

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinachofaa kuliwa na kutoleta madhara kwa binadamu;

"Eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo yote yaliyoamriwa na Halmashauri ya Wilaya au Halmashauri ya kijiji kuwa yatakuwa ni eneo la hifadhi. Maeneo hayo ni hifadhi ya misitu, ardhi oevu, vyanzo vya maji, milima, hifadhi ya barabara, hifadhi ya mbuga za wanyama, hifadhi ya milima, hifadhi ya ardhi kwa ajili ya huduma za jamii na maeneo ya makaburi.

"Kelele" ni kila aina ya uchafuzi au usumbufu usababishwao na sauti ambayo iwezayo kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu na mazingira;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

"Hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji wa ardhi, mimea na viumbe wegine Halmashauri kama hifadhi kama vile maeneo ya misitu, mabonde, vyanzo vya Maji, hifadhi ya barabara, hifadhi ya maeneo ya makaburi, milima;

"Jengo" maana yake ni nyumba, kibanda, kontena na hema;

"Kibali cha ujenzi" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa chini ya sheria ndogo hizi kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa jengo

"Madini" maana yake ni aina yoyote ya mali zinazochimbwa ardhini ikiwa ni pamoja na mchanga, mawe, kokoto, dhahabu, galena zink na udongo.

"Makazi" ni pamoja na nyumba, kiwanja na kila aina ya miliki ikiwa ni pamoja na mashine, mitambo au gari litumikalo katika kazi yoyote ifanywayo katika makazi hayo;

"Mamlaka" maana yake ni mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

"Mazingira" yanahusisha maumbile halisi yamzungukayo binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, hali za kibaolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya kiuchumi, kijamii, majengo na mambo mengine yaliyoundwa au kutengenezwa na binadamu na yale ya asili;

"Mfumo wa utalii" maana yake ni maeneo yote ya Halmashauri yaliyohifadhiwa au kuainishwa kwa ajili ya utalii;

"Mifugo" ni pamoja na ng'ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe, kuku, farasi, mbwa, punda na wanyama wengine wanaofugwa na kudhibitiwa na binadamu;

"Misitu" inahusisha ardhi yenye uoto wa mimea na uwingi wa miti ya kilimo

chochote ivunwayo na isiyovunwa;

"Mkurugenzi" maana yake ni mtendaji Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

"Mpango wa ujenzi" maana yake ni mpango wa ujenzi ulioandaliwa na Halmashauri unaoeleza aina ya jengo la kujengwa katika eneo lolote la kiwanja au shamaba lililopo ndani ya Halmashauri;

"Rasilimali za mazingira" ni pamoja na rasilimali za hewa, ardhi, maji, misitu na uoto mwingine wa asili, wanyama na mimea;

"Sheria" maana yake ni Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Taka hatarishi" maana yake ni taka ngumu, miminika na hewa ambazo zina kiwango kikubwa cha kemikali ambazo husababisha sumu na kuathiri maisha ya binadamu pamoja na mazingira kwa ujumla wake;

"Uchimbaji wa madini" maana yake ni kuchimba, kuchenjua madini (plants), utafiti wa madini pamoja na uchomaji wa madini(elution);

"Udongo" hujumuisha ardhi, mchanga, mwamba, mwambatope, madini, uoto, mimea na viumbe waishio humo na vyote vitokanavyo kama vile vumbi;

"Uharibifu" maana yake ni mabadiliko ya moja kwa moja ya rasilimali za kimaumbile, hali ya joto, kemikali, kibaolojia ambazo ni sehemu ya mazingira na hivyo kuleta madhara kwa matumizi yenye manufaa, au kusababisha hali ambayo ni hatari kwa jamii kiafya, kiusalama au ustawi wa binadamu na mazingira;

"Ujenzi" ni kuanzisha/kujenga jengo jipya pamoja na ukarabati wa jengo;

"Usimamizi wa mazingira" ni pamoja na kulinda, kuhifadhi na kutumia kwa njia endelevu sehemu ya rasilimali ya mazingira.

"Vyanzo vya maji" maana yake ni pamoja na chemchem, mito, mabwawa,ardhi oevu, kisima, mabonde ya mito na maeneo ya milima;

"Zizi" maana yake ni jengo maalum kwa ajili ya matumizi ya kufugia mifugo.

## SEHEMU YA II

## HIFADHI YA ARDHI YA MISITU NA VYANZO VYA MAJI

*Upandaji miti na utunzaji miti*

**4**. -(1) Litakuwa ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba:-

(a) Inatenga eneo maalum kwa ajili ya kuotesha miche ya miti ambayo itapandwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa utaratibu utakaopangwa.

(b) Inatenga eneo au maeneo kwa ajili ya kupanda miti au kutunza miti

iliyokwisha pandwa kama hifadhi ya misitu na hakuna shughuli zozote zitakazoruhusiwa kufanyika katika eneo au maeneo hayo.

(c) Inasimamia utunzaji wa rasilimali za misitu iliyomo katika mamlaka yake.

(d) Inasimamia kampeni za vijiji na Wilaya kwa ujumla kupanda miti na kuhifadhi mazingira.

(e) Inapanga siku moja au zaidi kwa kila mwaka kwa ajili ya kupanda miti ambapo watu wote watakaotakiwa kushiriki katika zoezi hilo watalazimika kufanya hivyo.

(f) Inatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mchanga kokoto, mawe, udongo, kifusi, kuoshea magari, karakana, mashine za mbao, na nafaka, na shughuli hizi zitafanywa baada ya kuomba na kupata kibali cha Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

(g)Inatenga maeneo maalumu ya kujenga elution, plants na viwanda

(h)Inatenga siku maalumu ya kuhifadhi na kusafisha mazingira

(2) Mmiliki yeyote wa ardhi atapaswa kupanda na kuhifadhi miti isiyopungua mitano katika eneo lake na mmiliki mpya wa ardhi hatapata kibali cha ujenzi hadi atakapo kuwa amepanda na kutunza miti isiyopungua mitano katika kiwanja chake kwa kuzingatia aina na maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri.

(3) Kila asasi na taasisi zilizomo ndani ya mipaka ya Halmashauri zitahakikisha kwamba:-

(a) Zinapanda na kutunza miti katika maeneo yaliyo chini ya uangalizi wao.

(b) Zinashiriki vema katika shughuli za kupanda miti na kuhifadhi mazingira pale watakapo takiwa kufanya hivyo.

(c) Zinatoa taarifa mara moja kwa mamlaka pale inapobainika kuwa kuna uharibifu wa mazingira katika maeneo yao.

*Shughuli za utalii*

(4) Taasisi au mtu yeyote atamiliki kitalu cha miti baada ya kupata kibali cha maandishi kutoka Halmashauri

**5**–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuwatembeza watalii katika maeneo ya hifadhi ya mazingira pasipo kupata kibali cha Halmashauri.

*Ukataji miti*

(2) Kampuni zote za kitalii zitaendeshwa kwa kufuata mfumo ulioainishwa katika mpango mahsusi wa utalii wa Halmashauri.

**6.** -(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata mti au sehemu ya mti pasipo kupata Kibali cha Halmashauri.

*Uwashaji moto*

(2) Halmashauri itatenga maeneo ya misitu ambayo miti itaruhusiwa kukatwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali baada ya kupata kibali cha Halmashauri.

**7**. -Mtu yeyote atakayewasha moto au kufanya au kutokufanya jambo ambalo litasababisha kuwaka moto katika maeneo ya misitu isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

*Ardhi hatarishi*

**8.** -(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi maeneo ambayo ni vyanzo vya maji, pembezoni mwa mito, visima vya maji, chemichemi za maji pamoja na miteremko ya milima ni maeneo ya ardhi hatarishi.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli zifuatazo katika maeneo yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu bila kupata kibali cha Halmashauri:-

a) Kuweka, kujenga, kurekebisha, kuondoa au kubomoa aina yoyote ya jengo.

(b) Kuchimba au kulima kwa madhumuni yoyote yale.

(c) Kupanda mmea au sehemu fulani ya mmea uwe wa asili au usio wa asili pasipo idhini ya Halmashauri.

(d)Kuchepusha maji ya mto au mfereji kutoka katika mkondo wake pasipo kibali cha Mamlaka.

(e) Kufanya shughuli za kilimo.

(f) Kupitisha barabara, njia au mfumo wowote wa miundombinu.

(g) Kuchunga mifugo au kupitisha mifugo

(h)Kuchimba madini ya aina yoyote

(I)Kuchimba udongo au mchanga kwa ajili ya kufyatua tofari

*Ufugaji*

## SEHEMU YA III

## TARATIBU ZA UFUGAJI WA MIFUGO

**9**.-(1) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kufuga mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

(2) Halmashauri itatoa kibali cha ufugaji baada ya kuridhika kwamba ufugaji huo hautakuwa kero kwa jamii na maeneo hayo hayawezi kuwa hatarishi.

(3) Ufugaji ambao utaruhusiwa katika maeneo ya mjini ni ule tu wa ndani ambao utakuwa umethibitishwa na Halmashauri.

(4) Katika kibali hicho Afisa Mifugo wa Halmashauri atataja aina na idadi ya mifugo inayoruhusiwa kufugwa kulingana na ukubwa wa eneo la mfugaji pamoja na masharti mengine ya usajili, upigaji wa chapa na chanjo ya mifugo.

*Usafi wa zizi*

(5) Kibali kitatolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

**10**.-(1) Kila mfugaji atahakikisha kwamba sehemu yake anayotumia kufugia mifugo inakuwa katika hali ya usafi wakati wote na anakuwa na shimo au chombo cha kuhifadhia uchafu unaozalishwa na mifugo yake.

(2) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kumtaka mfugaji kuondoa uchafu wowote ule uliopo kwenye jengo analotumia kufugia.

*Usafirishaji wa mifugo*

(3) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika jengo lolote lile bila taarifa linalotumiwa kwa kufugia kwa lengo la kukagua usafi, chanjo, na chapa

**11**.-(1) Hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kusafirisha mfugo wake kutoka katika sehemu moja ya Halmashauri kwenda katika sehemu nyingine bila ya kuwa na kibali kutoka Halmashauri.

Hata hivyo sheria hii haitahusu mifugo inayokwenda katika machinjio ambayo itakuwa inasafirishwa kwenye gari au ambayo ina kibali kilichotolewa na Serikali.

*Kuhamisha mifugo*

(2) Kibali cha kusafirisha mifugo kutoka katika sehemu moja kwenda nyingine kitadumu kwa mujibu wa sheria na kitalipiwa kadri itakavyoelekezwa na Halmashauri na serikali kwa ujumla.

**12**.-(1) Mkurugenzi wa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi anaweza kuamuru

mifugo ihamishwe kutoka katika sehemu inayofugiwa iwapo ufugaji huo unakinzana na sheria za mipango miji hivyo kuwa kero kwa wakazi wa eneo husika au wakulima wa mazao.

*Udhibitii mifugo*

(2)Iwapo Mkurugenzi atatoa amri hiyo Halmashauri haitahusika na gharama wala hasara ambayo mfugaji atakuwa amepata.

**13**. –(1) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata mifugo ambayo:-

(a) Inafugwa bila kuwa na usajili na kupewa kadi maalumu ya mifugo
(b)Inafugwa bila kupigwa chapa ya utambuzi ya Halmashauri;
(c) Inafugwa nje ya jengo la kufugia;
(d) Inasafirishwa bila ya kuwa na kibali cha kusafirishia
(e) Inazurura katika eneo la mji au kijiji bila kibali.
(f)Inachungwa/kulishwa kwenye eneo la Hifadhi au maeneo mengine yasiyoruhusiwa

(2) Pasipo kuathiri kifungu kidogo cha (1) hapo juu Halmashauri inaweza kuchukua uamuzi wa kuua mbwa wataokutwa wanazurura ovyo mitaani pasipo kuwa na kibali cha Halmashauri.

*Faini za mifugo*

**14**.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo kutoza faini kupitia mifugo iliyokamatwa kwenye hifadhi na maeneo mengine yasiyoruhusiwa. Viwango vya faini kwa kila mfugo uliokamatwa itakuwa kama ilivyoainishwa katika jedwali la Sheria ndogo hizi.

**JEDWALI "A"**
**VIWANGO VYA FAINI /ADHABU KWA MIFUGO ILIYOKAMATWA**

| NA | AINA YA MIFUGO | IDADI YA MIFUGO ILIYOKAMATWA | VIWANGO VYA FAINI KWA KILA MFUGO ULIOKAMATWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Kwa kila Ng'ombe aliyekamatwa | 50,000/= |
| 2. | Punda | Kwa kila Punda aliyekamatwa | 40,000/= |
| 3. | Mbuzi | Kwa kila Mbuzi aliyekamatwa | 30,000/= |
| 4. | Kondoo | Kwa kila Kondoo aliyekamatwa | 30,000/= |
| 5. | Nguruwe | Kwa kila Nguruwe | 20,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | aliyekamatwa | |
| 6. | Wanyama wengine | Kwa kila mnyama aliyekamatwa | 15,000/= |

(2) Endapo mtu anayemiliki mifugo iliyokamatwa atashindwa kulipia mifugo yake ndani ya siku tatu kuanzia siku ya kukamatwa mifugo hiyo basi itakuwa ni halali kwa Mkurugenzi Mtendaji kutoa idhini ya kuruhusu mifugo hiyo iuzwe katika mnada wa hadhara au kupeleka mahakamani ili mahakama itoe amri ya faini kama ilivyoanishwa hapo juu kwenye jedwali la kifungu 14 (1) cha sheria hii. Na mtu huyo atalazimika kulipa pamoja na gharama za ukamataji ambayo itakuwa ni asilimia ishirini ya faini ya kila mfugo. Au kuruhusu mifugo iuzwe kisha mmiliki kufungwa kifungo jela cha miezi kumi na mbili.

(3) Endapo mifugo iliyokamatwa haijulikani mmiliki wake au mwenye mifugo ameshindwa kujitokeza ndani ya siku tatu basi Mkurugenzi Mtendaji atauza kwa mnada mifugo hiyo. Iwapo mwenye mifugo amejitokeza wakati wa mnada au ndani ya siku tatu baada ya mnada kufanyika basi atarudishiwa fedha zinazozidi kiwango cha faini kilichoainishwa kwenye jedwali la kifungu 14 (1) cha sheria hii.

(4) Halmashauri haitahusika na kifo, ugonjwa, hasara na upotevu wowote ule wa mifugo itakayo kamatwa.

*Kuzuia kilimo maeneo ya kuchunga*

**15**. - Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuanzisha shughuli za kilimo kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuchunga au kulisha mifugo.

## SEHEMU YA IV

## SHUGHULI ZA UCHIMBAJI NA UCHENJUAJI WA MADINI

*Utaratibu wa uchimbaji wa madini, mawe udongo, mchanga na kokoto*

**16**. -(1) Ili kuzuia uharibifu wa ardhi na mmomonyoko wa udongo itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kuchenjua madini, mawe, udongo, kokoto kwa ajili ya matumizi yoyote yale au kumiliki eneo kwa ajili ya shughuli yoyote kwenye maeneo ya hifadhi pasipo kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayepewa kibali cha kuchimba kuchenjua madini, mawe, Mchanga, kokoto au kufyatua tofali au kuchoma tofali hizo, ataruhusiwa kufanya shughuli iliyokusudiwa tu na si vinginevyo .

*Ujenzi wa planti*

*elution na karasha*

**17** -(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi shughuli zote za uanzishwaji wa planti na Ya kuchenjua madini, Elution au karasha la kusaga mawe zitafanyika baada ya Kupata kibali cha halmashauri na kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na Afisa anayehusika.

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuhusika katika kufanya shughuli za madini katika Eneo lolote bila vibali atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi

*Uharibifu wa barabara*

**18**.- (1) Ni marufuku kwa mchimbaji au mtu mwingine yeyote:-

(a) kukata, kuweka matuta na vizuizi vingine katika eneo lolote la barabara;

(b) kufanya uchafuzi wa aina yoyote katika eneo la barabara; na

(c) kuingiza maji machafu katika mifereji ya barabara.
(d)kuchimba madini kwenye maeneo ya barabara
(e)kupitisha magari mazito yanayozidi tani 8 kwenye barabara ndogo bila kibali cha Halmashauri au TARULA
(f)kupaki/kuegesha magari maeneo yasiyoruhusiwa
(g)kuondoa alama za barabara au bango lolote lililowekwa kisheria
(i)kupitisha magari bila kuzingatia taratibu za kutoka na kuingia kwenye barabara
(j)kuweka bango au tangazo kandokando ya barabara bila kibali cha halmashauri
(k)kupitisha mtambo wowote au kitu chochote kinachokwangua au kuharibu barabara

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu miundombinu ya aina yoyote, kalvati, kujitengenezea mifereji ya maji au namna yoyote itakayoharibu maji

*Ujenzi kwenye eneo la barabara*

**19**.-(1) Mtu yeyote ambaye atakuwa amejenga au ameweka kibanda/jengo barabarani atatakiwa kuondoa au kubomoa ujenzi huo baada ya kupewa taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne kwa gharama zake mwenyewe.

(2) Iwapo baada ya kupewa taarifa ya siku kumi na nne mtu huyo atashindwa kutekeleza amri hiyo, Halmashauri itabomoa na kumpelekea gharama za ubomoaji huo mhusika na kuwajibika kulipa gharama hizo na faini ya laki tatu

*Shughuli za kilimo kwenye maeneo ya mji*

**20**. Ni marufuku kuendesha shughuli za kilimo cha mazao marefu ya zaidi ya futi tatu katika maeneo yote ya miji ya Halmashauri na kama itabidi ni baada ya kupata kibali cha Halmashauri. Mtu yeyote atakayekutwa atapewa notisi ya siku kumi na nne kuteketeza mazao yake akikaidi Halmashauri itateketeza na kumdai gharama za kuteketeza pamoja na kumshitaki.

**21**. –(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya mambo yafuatayo:-

*Biashara ya madini*

(a) Kufanya biashara ya madini bila ya kuwa na vibali na leseni kutoka katika Ofisi ya Halmashauri.

(b)Kufanya biashara nje ya maeneo yasiyoruhusiwa pasipo kupata kibali maalumu ambacho kitatolewa na halmashauria au Ofisi za madini

(2) Kwa madhumuni ya sheria ndogo hii na pasipo kuathiri vifungu vya Sheria Ndogo hii hairuhusiwi kusafirisha au kuuza madini usiku kuanzia saa 1.00 jioni hadi saa 1.00 asubuhi.

*Kitalu cha madini*

**22**. -Itakuwa ni ukiukwaji wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote atabainika kutumia kitalu cha madini:

i. Bila kulipia ada ya kila mwaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

ii. Kubadilisha matumizi ya kitalu kinyume na masharti ya matumizi ya machimbo au uchenjuaji au elution au shughuli nyingine ya madini

iii. Kukodisha kitalu cha madini au kumuuzia mtu mwingine bila taarifa kwenye Halmashauri.

*Udhibiti wa mazingira kwenye maeneo ya uchimbaji*

**23**. -(1) Kutakuwa na Kamati ya Mazingira kwa kila Kata na Vijiji itakayohusika na usimamizi wa mazingira kwa Kata na Vijiji husika ambayo itakuwa pia inapita kukagua shughuli za uchimbaji wa madini

(2) Afisa mwidhiniwa au Kamati katika kusimamia mazingira itashirikiana na askari mgambo kupita na kukagua usafi wa mazingira, choo, hifadhi ya takataka, mitaro ya maji, ufyekaji wa majani, utunzaji wa mifereji ya kutiririsha maji na iwapo itabaini ukiukwaji wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni halali kutoza papo kwa papo faini isiyopungua laki moja kwa kila kosa au kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo na faini ya laki tatu.

(3) Mtu yeyote atakayekaidi kulipa faini chini ya kifungu cha (2) hapo juu, atashitakiwa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Hifadhi ya maji kwenye*

**24**. -(1) Ili kuepuka uharibifu unaoweza kujitokeza katika maeneo ya machimbo ya madini na maeneo mengine ya wazi itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kufanya kuosha madini kwenye vyanzo vya maji, kuosha vyombo vya usafiri au mitambo katika maeneo ya vyanzo vya maji.

*maeneo ya machimbo*

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii si ruhusa kwa mtu yeyote kujisaidia haja ndogo au kubwa eneo lolote lile isipokuwa katika sehemu iliyoandaliwa kwa matumizi hayo.

(3) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kuvunja kifungu kidogo cha (1) na (2) hapo juu, pamoja na adhabu nyingine atakayopewa pia atalazimika kulipa fidia kutokana na uharibifu atakaosababisha kwenye chanzo cha maji au eneo husika.

(4) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuondoa mtambo au chombo chochote cha machimbo ambacho ni kibovu kinachoweza kuharibu mazingira

*Udhibiti wa machimbo holela*

**25.** –(1) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kujenga planti, elution au namna nyingine ya kuzalisha madini pasipo kwanza kukaguliwa eneo na kupatiwa vibali vya usajili au kupata cheti cha tathmini ya athari ya mazingira.

(2) Mtu yeyote atakayejenga mtambo wowote wa madini kabla ya kuruhusiwa cha atakuwa ametenda kosa na anaweza kulazimishwa kubomoa na kulipa faini ya shilingi laki tatu.

## SEHEMU YA V
## UDHIBITI WA UCHAFUZI WA HEWA

*Shughuli za viwanda na vyombo vya usafiri*

**26**. -Ili kuepuka madhara ambayo binadamu anaweza kupata kutokana na hewa chafu ni marufuku mtu yeyote:

(a) Kufanya shughuli yoyote inayoweza kuzalisha moshi na hewa chafu katika maeneo ya makazi, maeneo ya ofisi, maeneo ya wazi, barabarani na maeneo ya biashara.

(b) Kuachia hewa chafu au kali hewani ambayo inaweza kuathiri mfumo wa anga na hewa.

(c) Kuendesha gari au mtambo chakavu ambao unatoa moshi mkali hasa katika makazi, barabarani na ofisini.

*Uzuiaji wa viwanda kutoa hewa*

**27**. –(1) Wamiliki wote wa viwanda watahakikisha kuwa:-

(a) Wanakagua mashine zao mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba zinafanya kazi vizuri na kuzuia moshi na hewa chafu;

(b) Mabomba ya kutolea moshi na hewa chafu yanafungwa vifaa maalum ili kuepuka na au kupunguza madhara kwa viumbe hai na mazingira; na

*chafu*

(2) Shughuli zote za viwanda ikiwa ni pamoja na karakana, mashine kubwa za kusaga na kukoboa na mashine za mbao zitafanyika tu katika maeneo yaliyotengwa kwa kazi hiyo ili kuepusha hewa chafu, vumbi, kelele na madhara mengine katika maeneo ya makazi na shughuli nyinginezo za binadamu isipokuwa kwa mashine ndogo za kusaga nafaka kwa umeme.

(3) Viwanda vyote vitatakiwa kuwa na cheti cha tathmini ya mazingira kilichotolewa na Serikali na kuorodheshwa kwa ukaguzi.

*Vyombo kuwa na hewa chafu na kelele*

**28**. –(1) Ni marufuku kupitisha vyombo vya usafiri wa barabara vitoavyo kelele kubwa katika maeneo yanayohitaji utulivu, hasa katikati ya mji, hospitali, ofisi za taasisi mbalimbali za serikali na makazi ya watu, na kama itaruhusiwa ni baada ya kupata kibali cha mamlaka.

(2) Halmashauri itachukua hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeendesha shughuli kama vile muziki, mihadhara, mahubiri, mnada na kufanya matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti kwa sauti ya juu na kusababisha kero kwa watu katika maeneo ya makazi na yale yanayohitaji utulivu mkubwa bila kupata kibali cha Mamlaka.

*Nyumba kuwa na hewa safi*

**29**. Kila mkazi wa Halmashauri atahakikisha kwamba nyumba yake inakuwa na:-

(a) Milango na madirisha ili kuruhusu hewa na mwanga wa kutosha; na

(b) Mfumo bora wa kupitisha moshi kutoka jikoni na maeneo mengineyo yanayotoa au kuzalisha moshi.

## SEHEMU YA VI
## UJENZI WA MAJENGO MBALIMBALI

Kudhibiti makazi holela

**30**. -(1) Bila kuathiri Sheria ya Mipango Miji hakuna mtu atakayeruhusiwa kujenga katika eneo la Halmashauri kabla ya kupata kibali kutoka Halmashauri.

(3) Gharama na masharti ya kibali cha ujenzi yatakuwa kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ndogo ya Ada na ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

(2) Pamoja na masharti mengine yatakayokuwemo katika kibali cha ujenzi, umbali kutoka katikati ya barabara na jengo litakalojengwa utakuwa ni Mita 13 kwa barabara kuu na mita 5 kwa barabara za mitaani.

*Kusajili ramani ya jengo*

**31**.-(1) Kutakuwa na mpango wa ujenzi ambao utaainisha aina ya nyumba za kujengwa katika maeneo ambayo yatakuwa yameainishwa katika mpango huo.

(2) Kila mtu atakayetaka kujenga atahakikisha kwamba jengo analotaka kujenga linaoana na mpango wa ujenzi.

*Usalama wa jengo*

**32**.-(1) Litakuwa ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba jengo pamoja na mazingira yake yanakuwa katika hali ya usafi wakati wote.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumtaka mwenye nyumba au mpangaji kukarabati nyumba ikiwa ni pamoja na kupaka rangi endapo nyumba hiyo itakuwa imechakaa.

*Kujenga kuzingatia kibali*

**33**.-(1) Kila mwenye nyumba au mpangaji atahakikisha kwamba hazuii barabara au njia inayotumiwa na umma katika eneo lake.

(2) Iwapo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria Ndogo hizi, kuna mtu alizuia barabara au njia ya umma itamlazimu kubomoa ujenzi huo kwa manufaa ya umma.

*Maombi ya kujenga kwa kibali Maalumu*

**34**.-(1) Halmashauri itahakikisha kwamba inajibu maombi yote ya kibali cha ujenzi ndani ya muda wa siku thelathini tangu siku ya kupokea maombi husika.

(2) Kama Halmashauri itashindwa kushughulikia maombi ya kibali cha ujenzi ndani ya muda wa siku tajwa, itamaanisha kwamba maombi hayo yamekataliwa

*Ilani ya Kujenga bila kibali*

**35**. Endapo kuna mtu ambaye atakuwa amejenga pasipo kuwa na kibali cha ujenzi, Halmashauri itampa ilani ili aweze kubomoa ujenzi huo ndani ya muda utakaotolewa katika ilani hiyo.

*Kubomoa jengo*

**36**. Baada ya mtu kupelekewa ilani ya uvunjaji na akashindwa kutekeleza uvunjaji huo huo Halmashauri itafanya ubomoaji na itamdai mwenye jengo gharama za ubomoaji wa jengo husika.

*Ufifilisha*

**37**. Mkurugenzi Mtendaji, Mwanasheria na Mtendaji Mkuu wa Mamalaka ya Mji Mdogo Makongolosi wanaweza kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kutenda kosa hilo kwa maandishi, mkosaji atalipa faini kwa mujibu wa sheria.

*Adhabu*

**38**. Isipokuwa kifungu 14 cha sheria hii, Mtu yeyote atakayevunja kifungu kingine chochote cha Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Kufutwa kwa sheria za awali*

**39**. Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2009; Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2015 zilizotangazwa katika gazeti la Serikali na 486 la tarehe 30/10/2015 zote kwa pamoja zimefutwa.

JEDWALI

(Limetungwa chini ya kifungu cha 37)

KUFIFILISHA KOSA

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya………………………………………ambaye ni Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji wa Mamlaka ya Mjimdogo Makongolosi kwamba mnamo tarehe………………………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Ardhi Mazingira na Uchimbaji wa Madini) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018. (Ambapo najutia kosa langu na kukiri kutorudia tena)

Kwahiyo kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, Mwanasheria au Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi niko tayari kugharimia uharibifu kiasi cha shilingi……………………….. pamoja na faini ya shilingi…………………………ambapo jumla shilingi……………………………..

Kiasi hicho kitalipwa siku ya tarehe……………………………… bila kukosa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YA HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU NA SIJALAZIMISHWA NA MTU AU AFISA YEYOTE.

Leo tarehe……………………………Nikiwa eneo la………................................

Saini……………………………Majina……………………………………Simu……

Kijiji/Kitongoji ninachoishi………………………Kata………………………………

Mbele ya:

Saini………………………………………..

Jina…………………………………………

Wadhifa……………………………………

TANGAZO LA SERIKALI Na……………la Tarehe………………

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 287)

**SHERIA NDOGO**

(Imetungwa chini ya kifungu Na. 153)

SHERIA NDOGO YA (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA) ZA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama *Sheria Ndogo ya (Uanzishaji wa Bodi ya Huduma za Afya) za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za mwaka 2018* na itaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

Tafsiri

**3.** Katika Sheria ndogo hii isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

“Afisa Afya wa Halmashauri” maana yake ni mtumishi wa afya ambaye ndiye mkuu wa utoaji wa huduma za afya msingi katika Halmashauri.

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Hati Rasmi hii.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

“Hospitali ya Halmashauri”maana yake ni hospitali ya ngazi ya kwanza iliyo katika Halmashauri ya Wilaya na iliyo na mamlaka ya kutoa huduma za afya za Halmashauri ya Wilaya ikiwa ni pamoja na kupokea wagonjwa wa rufaa toka ngazi za chini.

“Hospitali Teule” maana yake ni hospitali binafsi ya ngazi ya kwanza ambayo ina mkataba maalumu na Serikali ambao unairuhusu hospitali hiyo kuendesha shughuli zake kama hospitali ya Wilaya kwa niaba ya Serikali.

“Kamati ya Afya ya Kata” maana yake ni kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 38 cha hati rasmi hii.

“Kamati ya maendeleo ya kata ” maana yake ni kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 20 cha sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 287

“Kamati ya Kituo cha Afya” maana yake ni kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 30(1) cha Hati Rasmi hii;

“Kamati ya Usimamizi ya Hospitali” maana yake ni kamati ambayo imeanzishwa chini ya kifungu cha 18 cha Hati Rasmi hii.

“Kituo cha Afya” maana yake ni kituo cha kutolea huduma ya afya ambacho kiko ndani ya Kata, kinatoa huduma za afya kwa wagonjwa wa nje na waliolazwa pamoja na waliopewa rufaa toka kwenye zahanati ikiwa ni pamoja ya Mama na mtoto na kina uwezo wa Vitanda kumi na tano na kuendelea.

“Kituo cha Huduma ya Afya cha Umma” maana yake ni kituo cha kutolea huduma ya afya kinasimamiwa na serikali.

“Kituo cha Huduma za Afya cha shirika lisilo la serikali” maana yake ni kituo cha huduma za afaya kinachomilikiwa na shirika au chama kwa misingi ya kujitolea na kutoa huduma na malipo bila faida na kinaendesha shughuli zake kwa kufuatana na kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali.

“Kituo cha Huduma za afya cha binafsi ” maana yake ni kituo cha Huduma za Afya kinachomilikiwa na kuendeshwa katika utoaji wa Huduma zake lengo likiwa ni pamoja na kupata faida.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji au Ofisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji” maana yake ni daktari ambaye ni msimamizi mkuu wa huduma za afya katika Halmashauri.

“Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri” maana yake ni timu ya kitaalamu ya uendeshaji wa shughuli za afya kwenye Halmashauri iliyoanzishwa chini kifungu cha 14 cha Hati Rasmi hii.

“Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa” maana yake ni timu ya wataalamu wa afya, inayosimamia shughuli zote za huduma za afya mkoani;

“Timu ya uendeshaji wa Huduma za Afya ya Hospitali” maana yake ni timu ambayo inawahusisha viongozi wataalam au wakuu wa sehemu au vitengo kwenye hospitali ya Wilaya

“Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Kituo cha Afya” maana yake ni timu ya viongozi wataalam au wakuu wa sehemu au vitengo na wakuu wa vituo vya afya;

‘’**Timu ya Uendeshaji ya Kata** ‘’ maana yake ni timu ya wataalum wa sekta mbalimbali wanaosimamia maendeleo ya wananchi ndani ya kata husika na kufuatilia utekelezaji wake ndani ya kata.

"Vituo vya Kutolea Huduma" maana yake ni pamoja na Hospitali, kituo cha afya, kliniki ya tiba, zahanati, maabara ya afya, kituo cha uzazi na uuguzi na pia vituo vingine vilivyoanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma za afya.

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana ya afya.

Sheria Na. 5 ya 1992

"Wadhifa wa kisiasa" maana yake ni kuwa na madaraka ya kuteuliwa au kuchaguliwa kwenye chama chochote cha kisiasa kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992.

"Zahanati" maana yake ni kituo cha kwanza kinachotoa huduma kinachotambulika na Halmashauri ambacho kipo ndani ya kata ambacho hutoa huduma kwa wagonjwa wa nje ikiwa ni pamoja na huduma za mama na mtoto na kinaweza kuwa na vitanda vinne kwa ajili ya uangalizi wa karibu wa wagonjwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne.

Bodi

**4**. (1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri.

(2) Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Halmashauri.

Wajumbe wa Mfuko wa Bodi.

**5.** (1) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:-

(a) wawakilishi wanne wa watumiaji wa huduma za afya ambao wawili kati yao ni lazima wawe ni wanawake;

(b) mwakilishi mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida na mmoja kwa watoa huduma binafsi bila faida, walio katika makubaliano ya kutoa huduma na Bodi; na

(c) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii

(d) Afisa Mipango wa Halmashauri;

(e) Mganga Mkuu wa Halmashauri, ambaye atakuwa Katibu wa Bodi ;

(f) mwakilishi mmoja toka hospitali ya Halmashauri ya Wilaya au hospitali teule; na mwanasheria wa Halmashauri

(g) Mwakilishi kutoka Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya Mkoa.

(2) Mwenyekiti atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa kifungu kidogo (1) (a), (b) na (c) hapo juu.

(3) Wajumbe waliotajwa katika aya (a) (b) na (c) mbali na wajumbe waliotajwa katika aya (d),(e),(f) na (g) za kifungu kidogo cha (1) watakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi ya Bodi.

(4) Wajumbe wengine wanaweza kualikwa kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo; lakini hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura au kufanya maamuzi.

Sifa za kuwa mjumbe wa Bodi.

**6** (1) Mtu anaweza kugombea nafasi ya ujumbe wa Bodi kama atakuwa na sifa zifuatazo :

(a) ni lazima awe raia wa Tanzania, Sharti hili si lazima kwa wajumbe kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali;

(b) awe na umri kuanzia miaka ishirini na moja (21) na kuendelea,

(c) awe amehitimu elimu ya sekondari; yaani kidato cha nne na kuendelea; na

(d) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa toka chama chochote cha siasa.

(e) awe mwanachama hai wa mfuko wa jamii

(f) Asiwe ametiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) Awe mkazi wa Halmashauri.

.

(2) Diwani na mfanyakazi wa Halmashauri, mbali ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za jamii, hatoruhusiwa kuwa mjumbe wa Bodi, kwa kuwa Bodi ni chombo cha Halmashauri katika masuala ya uwajibikaji na tathmini.

Utaratibu wa kupata wajumbe wa Bodi

**7** (1)

(a) Uhamasishaji ushirikishe viongozi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla katika ngazi ya Wilaya, Kata au vijiji.

(b) Halmashauri kutoa matangazo ya nafasi za wajumbe wa Bodi kupitia Wilaya, Kata au vijiji

(c) Uchaguzi wa awali: Maombi ya nafasi yatawasilishwa kwenye mtaa/kijiji na uchaguzi utafanyika katika mkutano wa hadhara na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa kata/kijiji husika.

(d) Uchambuzi wa maombi: Orodha ya waombaji waliochaguliwa yatapelekwa kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa uchambuzi wa awali kwa kuzingatia sifa na mapendekezo yatapelekwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

(e) Uchambuzi wa majina ya wajumbe kutoka ngazi ya Kata yatafanywa na Timu ya Uendeshaji ya Afya ya Halmashauri ya Mji kwa kuzingatia sifa na mchakato wa uteuzi wao na kuwasilisha kwenye Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri, timu hiyo itahakiki na kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii na hatimaye Baraza la Madiwani kuidhinisha.

(f) Uzinduzi rasmi utafanywa na Mkuu wa Wilaya baada ya kupata Hati Rasmi iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kipindi cha kushika madaraka Bodi

**8.** (1) Wajumbe wa Bodi watakuwa katika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, kutoka tarehe ya ufunguzi na wataondoka baada ya muda huo lakini wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu;

(2) Mwisho wa kipindi cha muda wa Bodi, Mkurugenzi atatangaza nafasi zilizo wazi na watu wenye sifa hizo watajaza fomu maalum za maombi na kuzirudisha kwenye Halmashauri katika kipindi kitakachotolewa. Aidha mchakato wa kuunda bodi mpya utaanza miezi sita (6) kabla ya ukomo wa bodi iliyopo.

(3) Mjumbe wa Bodi anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu wa Bodi.

(4) (a) Pale ambapo nafasi katika Bodi itakuwa wazi kutokana na kifo, kujiuzulu, ugonjwa, au ulemavu utakaomzuia mtu huyo kushiriki kikamilifu au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kuziba nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.

(b) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha 4 (a), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita (6)

(5) Mjumbe atakayechaguliwa kutokana na kifungu kidogo cha (4) hapo juu, anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(6) Uchaguzi wa mwisho wa wajumbe waliochaguliwa kutoka kila mtaa utafanywa na Kikao Kikuu cha Halmashauri kupitia Kamati ya Uchumi na huduma za jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

(7) Bodi itazinduliwa rasmi na Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Kikao cha baraza la Madiwani.

(8) Endapo Bodi itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itaionya au kuivunja na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi mitatu tangu kuvunjwa.

(9) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote watapoteza nafasi zao.

(10) Katika kipindi ambacho Bodi imevunjwa, Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itasimamia shughuli zote za Bodi hadi hapo Bodi mpya itakapoteuliwa.

Vikao vya Bodi **9.** (1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka, na vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti au Makamu wake;

(2) Katibu ataitisha kikao maalumu kitakachokuwa cha kawaida cha Bodi kwa maombi yaliyoandikwa na kusainiwa na wajumbe wa bodi wasiopungua theluthi moja na pale inapohitajika.

(3) Mjumbe yeyote ambaye, bila taarifa au sababu ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi basi atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe na Halmashauri itatangaza nafasi wazi kwenye nafasi hiyo.

Akidi ya kikao **10.** (1) Nusu ya wajumbe wote wa kuchaguliwa ndiyo itakuwa akidi ya vikao vyote vya Bodi akiwemo Mwenyekiti au Katibu;

(2) Maamuzi ya idadi ya wajumbe wengi na waliopiga kura ndiyo yatakayokuwa maamuzi ya Bodi.

(3) Upigaji wa kura za siri ndiyo utakuwa utaratibu wa kufikia maamuzi katika vikao vya Bodi.

(4) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na pale ambapo itatokea kura kufungana, basi Mwenyekiti wa Bodi atakuwa na kura ya ziada mbali ya kura yake ya kawaida.

Majukumu na Kazi za Bodi

**11.** (1) Majukumu na kazi za Bodi zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) itahakikisha kuwa jamii inapata huduma bora za afya ambazo inazimudu na zitakazoimarisha afya zao;

(b) itahakikisha kuwa kuna upatikanaji wa rasilimali na mgawanyo wake, kwa kuzingatia mahitaji ya ngazi zote za huduma ya afya na matumizi bora;

(c) itajadili na kurekebisha mipango ya afya na bajeti na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa;

(d) itapokea, itachambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji kutoka kwa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri;

(e) itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendesha huduma za afya katika Halmashauri;

(f) itashirikiana na Kamati za Afya ndani ya Halmashauri,

(g) itaratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya afya katika Halmashauri; na

(h) itahakikisha kuwa kunakuwepo wafanyakazi wa kutosha kulingana na ikama ya Halmashauri;

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maelekezo ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Uhusiano wa Bodi na wadau na mamlaka nyingine

**12.** Uhusiano wa Bodi na jamii, wadau na mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo;

(a) Bodi itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia, kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za afya;

(b) Bodi itawajibika mbele ya Halmashauri ambapo:-

   (i) Mipango ya afya ya robo mwaka na mwaka pamoja na taarifa za kitaalam na fedha zinapitiwa na Kamati ya Uchumi, Huduma za Jamii na Kamati ya Fedha na Utawala, na baadaye kuthibitishwa na Baraza la Madiwani;

   (ii) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuza ufanisi kwa Halmashauri na vyombo vyake vingine vya utendaji bila ya Halmashauri kuingilia uhuru wa Bodi;

(c) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa ni chombo cha kitaalamu katika utekelezaji wa maamuzi ya Bodi;

(d) Kuhusiana na Kamati ya Uchumi na Huduma za jamii:

   (i) mipango yote na taarifa za maendeleo zitapitia katika Kamati hii, kwa hiyo kamati itakuza uhusiano;

   (ii) uhusiano na sekta nyingine utakuzwa na Bodi hasa katika utekelezaji wa maamuzi ya pamoja katika mambo muhimu kwenye Halmashauri;

(e) uhusiano na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, watoa huduma binafsi na wahisani:

   (i) kuwepo kwa wajumbe toka kwenye vyama vya hiari, mashirika yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi ndani ya Bodi kutaleta uhusiano mzuri baina yao;

   (ii) Bodi itashiriki katika utafutaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo Halmashauri, vyama vya hiari, jamii na wahisani;

(f) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa itatoa msaada wa kitaalamu na ushauri; na

(g) Jukumu la wizara zenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Afya litakuwa ni kuandaa sera ufuatiliaji na kuratibu shughuli za Bodi.

Vyanzo vya mapato vya Bodi

**13.** (1) Vyanzo vya mapato ya Bodi vitakuwa kama ifuatavyo:

(a) michango ya watu binafsi;

(b) Mfuko wa Afya ya Jamii(CHF)

(c) ada za watumiaji huduma; - papo kwa papo

(d) makusanyo toka Halmashauri;

(e) Wahisani na washirika,

(f) ruzuku toka Serikali Kuu; na

(g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

(h) Vyanzo vingine halali vya mapato

(2) Bodi itakuwa na akaunti maalum ya Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) ambayo itatunza fedha zitokanazo na michango.

(3) Wawekaji saini wa akaunti maalumu ya Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) pamoja na taratibu nyingine za Mfuko huo zitakuwa kama itakavyoelezwa Katika Sheria Ndogo za uanzishaji Mfuko wa Afya ya Jamii, (Tiba kwa Kadi).

(4) Halmashauri itaajiri au kuteua wahasibu wawili watakao simamia akaunti za afya.

(5) Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji, atakuwa ndiye mwanzishaji wa malipo yote.

(6) Akaunti hii itakaguliwa kufuatana na taratibu za Fedha za Serikali za Mitaa

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri

**14.** Kutakuwa na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri.

**Wajumbe**

**15.** Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao;

(a) Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya

(b) Katibu wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya

(c) Muuguzi Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya

(d) Afisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya

(e) Mfamasia wa Halmashauri ya Wilaya

(f) Fundi Sanifu wa Maabara wa Halmashauri ya Wilaya

(g) Daktari wa Meno wa Halmashauri ya Wilaya

(h) Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya

**Majukumu na kazi za Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya**

**16** (1) Majukumu na kazi za Timu ya Uendeshaji wa Huduma za afya ya Halmashauri zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) (a) kuandaa mipango kabambe ya afya ambayo itatilia mkazo mahitaji yote ya afya ya Halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango wa Afya wa Halmashauri;

(b) kuhakikisha kuwa hospitali, vituo vya afya na jamii vinatekeleza shughuli za afya kama inavyoelekezwa katika mpango kabambe wa Afya wa Halmashauri;

(c) kuhakikisha upatikanaji wa usafiri, dawa muhimu, chanjo, dawa, vifaa tiba, kemikali za maabara katika hospitali, vituo vya afya na zahanati

(d) kuwa tayari kukabiliana na magonjwa ya milipuko, maafa na kupanga mipango ya kudhibiti na kuzuia mambo hayo;

(e) kuhakikisha kuwa watumishi wa afya walio katika ngazi mbalimbali kwenye Halmashauri wanapata nyenzo za kuwawezesha kufuatilia utekelezaji wa shughuli za afya;

(f) kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kulingana na viwango vya Kitaifa;

(g) kuhakikisha kuwa watumishi wa afya wanakusanya takwimu, wanazichambua na kuzitumia katika mipango yao na kutoa mrejesho;

(h) kutambua maeneo ya kuweka kipaumbele, kusimamia na kufanya utafiti wa utendaji kazi katika Halmashauri ;

(i) kujumuisha na kuchambua taarifa za utekelezaji wa kitaalamu na fedha za robo mwaka na mwaka, halafu kuziwasilisha kwenye Bodi na sekretarieti ya Mkoa kupitia kwa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa;

(j) kusimamia mikutano ya wataalamu wa afya wanaotoa huduma za afya kwenye Halmashauri ili kuweza kutambua na kuratibu shughuli zote za afya;

(k) kusimamia na kusaidia utoaji wa huduma za afya ambazo ziko mbali kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma; na

(l) kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa shughuli za afya kwenye Halmashauri

(2) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itawajibika kwa Halmashauri.

Uhusiano wa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri na Kamati au mamlaka nyingine

**17** Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri, kwa madhumuni ya kuleta uongozi bora, itashirikiana na Kamati nyingine za afya na mamlaka nyingine ili kuleta mtandao wa utoaji wa huduma bora za afya katika Halmashauri.

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

**18.** Kutakuwa na Kamati ya Usimamizi ya Hospitali katika kila hospitali iliyo chini ya Halmashauri.

Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

**19** (1) Wajumbe wa kamati ya Usimamizi ya Hospitali watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) wawakilishi watatu kutoka watumiaji wa huduma za hospitali angalau mmoja awe ni mwanamke.

(b) wajumbe wawili kutoka kwenye kamati za vituo vya afya na zahanati za serikali

(c) mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi bila faida;

(d) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida.

(2) Kutakuwa na Sekretarieti ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao;-

(a) Mwakilishi toka Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji

(b) mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya, ambaye atakuwa Katibu; na

(c) Muuguzi mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya.

(d) Mwakilishi mmoja toka katika ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya

(3) Theluthi moja ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi lazima wawe ni wanawake.

(4) Wajumbe waliotajwa katika kifungu kidogo (1) hapo juu ndiyo watakaokuwa na haki ya kupiga kura.

(5) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati watachaguliwa kutokana na wajumbe wa kifungu kidogo cha (1) hapo juu;

(6) Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Hospitali anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu.

(7) Kamati ya Usimamizi wa Hospitali inaweza kumkaribisha mtu yeyote kuhudhuria vikao vyake kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo, lakini mtu huyo hatoruhusiwa kushiriki katika kupiga kura au kupitisha maamuzi ya Kamati.

Sifa za wajumbe wa Kamati ya usimamizi ya Hospitali

**20** Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe raia wa Tanzania, sharti hili halitawahusu wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali;

(b) Awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja na kuendelea

(c) Awe amehitimu elimu ya sekondari au zaidi

(d) Awe na akili timamu;

(e) Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya.

(f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa.

Taratibu za uchaguzi

**21** (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) cha kifungu hiki, wajumbe wote wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali watachaguliwa kwa kuzingatia sifa zao na kwa uwazi.

(2) Nafasi za uongozi katika Kamati ya Usimamizi ya Hospitali zitatangazwa katika gazeti linalopatikana katika Halmashauri pamoja na kutangazwa katika mbao za matangazo na mikusanyiko ya watu na watu wenye sifa zinazohitajika na wenye nia ya kufanya hivyo watapeleka maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri;

(3) Uchaguzi wa wajumbe utafanyika kwenye mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kata au afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri;

(4) Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara;

(5) Baada ya uchaguzi, orodha ya wajumbe waliochaguliwa itachanganuliwa na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na itapelekwa kwa Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri;

(6) Uteuzi wa mwisho utafanywa na Baraza la Madiwani kupitia Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

(7) Wajumbe wenye sifa zinazohitajika ndiyo watachaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali.

Uzinduzi rasmi

**22** Kamati ya usimamizi ya Hospitali itazinduliwa ramsi sanjari na uzinduzi wa Bodi ya Halmashauri

Muda wa kukaa madarakani

**23** (1) Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu na si zaidi ya vipindi viwili.

(2) Endapo Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itashindwa kutekeleza majukumu yake basi Halmashauri inaweza kutoa onyo au kuivunja.

Vikao vya Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

**24.** (1) Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu katika sehemu, tarehe na muda utakaopangwa na Mwenyekiti kwa kushirikiana na Katibu.

(2) Mwenyekiti wa Kamati kwa kushirikiana na Katibu wake anaweza kuandaa kikao cha dharura kama itakavyohitajika.

(3) Taarifa ya Kikao itapelekwa kwa kila mjumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali wiki moja kabla ya kikao kuanza, baada ya kuwafahamisha kwa maandishi madhumuni, tarehe na muda wa kikao.

**Majukumu na kazi za Kamati ya Usimamizi ya Hospitali**

**25.** 1 Majukumu na kazi za Kamati zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) itasimamia rasilimali za hospitali ,

(b) itapokea, itajadili na kupitisha mapendekezo ya mipango ya hospitali na bajeti na kuipeleka Halmashauri kwa ajili ya kuthibitishwa kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri,

(c) itapokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizoandaliwa na Timu ya Usimamizi ya Hospitali,

(d) itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kuendesha huduma za afya,

(e) itashirikiana na Kamati nyingine za afya na mashirika mbalimbali katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya,

(f) itapendekeza kuhusu upatikanaji wa watumishi na mafunzo yao ili kuleta ufanisi katika hospitali, na

(g) kutoa mrejesho kwa jamii kuhusu uendeshaji wa hospitali na mipango ya maendeleo.

**Utoaji taarifa na uwajibikaji**

**26.** Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itatoa taarifa na kuwajibika mbele ya Halmashauri kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri.

**Uhusiano wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali na Kamati au mamlaka nyingine**

**27**. Kamati ya Usimamizi ya Hospitali, kwa madhumuni ya kuleta uongozi bora, itashirikiana na Kamati nyingine za afya ili kuleta mtandao wa utoaji wa huduma bora za afya katika Halmashauri.

**Vyanzo na usimamizi wa mapato**

**28.** (1) Vyanzo vya mapato vya Kamati ya Usimamizi ya Hospitali vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) fedha itakayotengwa kwa ajili ya hospitali katika bajeti ya Halmashauri zilizopatikana kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri,

(b) mapato yatokanayo na uchangiaji wa huduma za afya yaliyotengwa na Bodi kwa ajili ya hospitali,

(c) ruzuku na michango itakayotolewa na Halmashauri, na Serikali Kuu; na

(d) vyanzo vingine halali vya mapato.

(2) Kutakuwa na akaunti ya hospitali ambayo itakaguliwa kwa kuzingatia kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa

(3) watia saini watakuwa katka makundi mawili kundi “A” Wataalamu na kundi “B” Jamii

(4) Mganga Mkuu wa Wilaya, atamteua mmoja wa wahasibu wake kusimamia akaunti ya Hospitali chini ya uangalizi wa Mganga Mfawidhi

(5) Mganga Mfawidhi ataanzisha hati zote za malipo zitakazohusiana na Shughuli za hospitali.

Bodi ya Hospitali Kufanya kazi za Kamati

**29.** Pale ambapo hakuna hospitali ya wilaya ya Serikali shughuli za kamati ya Usimamizi ya Hospitali zifanywa na Bodi ya usimamizi ya Hospitali Teule.

Kamati ya Kituo cha Afya

**30.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Kituo cha Afya, ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida;

(b) Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu;

(c) Wawakilishi watatu watumiaji wa huduma za Kituo watakaochaguliwa mmoja kutoka kila kata; pale ambapo kuna kata zaidi ya tatu, basi wataingia kwa kupokezana.

(d) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi bila faida;na

(e) Mtaalam mmoja kutoka kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu (c), mwakilishi wa kupokezana atakaa kwenye Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(3) Kamati ya Kituo cha Afya inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Kamati kuhudhuria katika vikao vyake, lakini mtu huyo hatashiriki katika kupiga kura au kutoa maamuzi ya Kamati;

(4) Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti watachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wanaopiga kura ;

(5) Theluthi moja ya wajumbe wote ni lazima wawe wanawake.

Sifa za Wajumbe

**31.** Mjumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya atapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe raia wa Tanzania, sharti hili haliwahusu wajumbe kutoka mashirika yanayotoa huduma za afya yasiyo ya kiserikali,

(b) Awe na umri si chini ya miaka ishirini na moja (21) na kuendelea

(c) Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya

(d) Awe na akili timamu.

(e) Awe amehitimu elimu ya msingi au zaidi na anajua kusoma na kuandika kwa kiswahili;

(f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) Asiwe na wadhifa wa kisiasa toka katika chama chochote cha siasa.

Taratibu za Uchaguzi

**32**. (1) Afisa Mtendaji wa Kata atatoa matangazo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya wawakilishi wa watumiaji huduma za vituo vya Afya na Zahanati

(a) Maombi yatafanyika kwenye mitaa akisimamia Mtendaji wa Mtaa na uchaguzi utafanyika kwenye mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja tu

(b) Uchambuzi wa waombaji kutoka katika kila Kata yatachambuliwa na Timu ya Uendeshaji ya kila Kata ambapo Kituo cha Afya na Zahanati ipo.

(c) Kamati ya Maendeleo ya Kata itafanya uchaguzi na kuwasilisha orodha ya wagombea wote kwenye Bodi ya Afya ya Halmashauri na Bodi itawasilisha kwenye Baraza la Madiwani kwa kuidhinishwa.

Muda wa kukaa madarakani

**33.** (1) Mjumbe wa kamati ya Maendeleo ya Kata mbali ya mwakilishi wa kupokezana, atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu isiyozidi vipindi viwili.

(2) Mjumbe wa Kamati anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu.

(3) Endapo mjumbe atajiuzulu nafasi yake itajazwa; na mjumbe atakayejaza nafasi hiyo atakaa kwenye uongozi kwa kipindi kilichobaki, lakini anaweza kuchaguliwa tena kuendelea kwa kipindi kingine.

(4) Mjumbe atakayejaza nafasi katika kifungu kidogo cha (3) hatoruhusiwa kufanya hivyo kama kipindi kilichobaki kitakuwa chini ya miezi sita.

(5) Iwapo Kamati ya Kituo cha Afya itashindwa kutekeleza majukumu yake basi Halmashauri inaweza kutoa onyo au kuivunja na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi mitatu.

Vikao vya kamati

**34** (1) Kamati ya Kituo cha Afya itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu katika sehemu, siku na muda utakaopangwa.

(2) Mwenyekiti wa Kamati kwa kushirikiana na Katibu anaweza kuandaa kikao cha dharura pale tu atakapoomba au kuombwa kufanya hivyo kimaandishi na kupata idhini ya wajumbe wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote.

(3) Katibu atatoa taarifa ya maandishi ya kikao kwa kila mjumbe wa Kamati wiki moja kabla ya kikao, kwa kumfahamisha madhumuni, siku na muda wa kikao.

Kazi za Kamati

**35.** (1) Kazi za Kamati ya Kituo cha Afya zitakuwa kama zifuatavyo:-

(a) itapokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizotayarishwa na Timu ya Uendeshaji wa Kituo cha Afya;

(b) itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendeshea huduma za Kituo cha Afya;

(c) kamati itashirikiana na washirika wengine katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya;

(d) itaimarisha miundombinu endelevu na usambazaji wa uhakika wa dawa na huduma za afya;

(e) itashauri na kutoa mapendekezo kwa Bodi kuhusu watumishi katika nyanja za ajira, mgawanyo, mafunzo, maendeleo na motisha;

(f) itasaidia Timu ya Uendeshaji ya kituo cha Afya katika kupanga na kusimamia mambo ya afya ya Jamii katika

eneo lake kama sehemu ya mpango wa Maendeleo ya kata; na

(g) itasimamia upatikanaji wa dawa muhimu, kemikali za maabara na vifaa tiba.

(2) Kamati ya Kituo cha Afya itawajibika kutokana na shughuli zake za kila siku kwa Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri

Vyazo vya mapato

**36**. (1) Vyanzo vya mapato vya Kituo cha Afya vitatokana na:-

(a) michango ya wananchi;

(b) wahisani na washirika;

(c) ruzuku toka Serikali Kuu;

(d) ruzuku toka Halmashauri; na

(e) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

(f) Na vyanzo vingine halali vya mapato

(h) Ada ya uanachama

(2) Mapato yote kwenye kituo cha afya yatahifadhiwa katika akaunti ya Kituo na kusimamiwa na Mganga Mfawidhi wa Kituo.

(3) Kamati ya Kituo cha Afya itawasilisha kwenye Bodi, mpango wa robo mwaka, nusu mwaka ambao baadaye utawasilishwa kwenye Baraza la Madiwani.

Uhusiano na taasisi nyingine

**37.** (1) Katika kutekeleza kazi zake, Kamati ya Kituo cha Afya:

(a) itahakikisha kuwa mahitaji ya afya ya jamii yanafanyiwa kazi;

(b) itatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ;

(c) itakuwa na daftari la usajili wa wachangiaji wa Mfuko wa Afya wa Jamii;

(d) itajenga na kuimarisha ushirikiano na uwiano na taasisi nyingine kwenye Halmashauri;

(e) itahakikisha kuwa Kamati ya Zahanati inawakilishwa kwenye Kamati ya Kituo cha Afya; na

(f) itahakikisha kuwa Kamati ya Kituo cha Afya inawakilishwa kwenye Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri;

(2) Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kituo cha Afya.

Kamati ya Afya ya Kata

Sura ya 409,

**38.** Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

Wajumbe wa Kamati
Sura 409 .

**39.** (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha kata husika;

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye shule ya msingi iliyopo kwenye Makao Makuu ya kata husika;

(d) Wajumbe wawili wanaoiwakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;

(e) Tabibu wa Afya Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi Msaidizi; wa kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;

(f) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa na serikali za mtaa zilizomo ndani ya eneo la kata; na

(g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii vilivyomo kwenye kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe hapo juu.

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itatoa onyo au kuivunja na kufanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

**40** Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Afya Kata zitakuwa ni kama zifuatavyo:-

(a) awe raia wa Tanzania, sharti hili haliwahusu wajumbe kutoka mashirika yanayotoa huduma za afya yasiyo ya kiserikali.

(b) awe na umri wa miaka ishirini na moja na kuendelea.

(c) awe na akili timamu

(d) awe na elimu ya msingi au zaidi na ajue kusoma na kuandika .

(e) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

(f) asiwe na wadhifa wa kisiasa toka chama chochote cha siasa

Kazi na majukumu ya Kamati

**41.** (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kuwahamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

(c) kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye huduma za afya;

(e) kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi;

(f) kuanzisha na kuratibu mipango ya Afya ya Jamii; na

(g) kuendesha mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.;

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu, na katibu atatoa taarifa ya maandishi wiki moja kabla ya siku ya Kikao.

(3) Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata watakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu na isiyozidi vipindi viwili.

Kamati ya zahanati

**42** Kutakuwa na kamati ya Zahanati.

Wajumbe wa Kamati ya Zahanati

**43** (1) Kamati ya Zahanati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) wajumbe wa kuchaguliwa ambao watapiga kura:-

(i) wajumbe watatu kutoka miongoni mwa jamii inayohudumiwa na zahanati husika angalau mmoja awe mwanamke.

(ii) mjumbe mmoja atakayewakilisha taasisi inayotoa huduma za afya bila faida;

(iii) mjumbe mmoja atakayewakilisha taasisi inayotoa huduma ya afya kwa faida;

(b) Kutakuwa na Sekretarieti ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i) mtaalam mmoja kutoka kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata;

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka kwenye Kamati ya Serikali ya Mtaa/Kijiji;

(iii) Mganga mfawidhi wa zahanati ambaye atakuwa Katibu, pale ambako kutakuwa na Zahanati zaidi ya moja, kutakuwa na utaratibu wa kupeana zamu;

(2) Idadi ya wajumbe wanawake si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote.

(3) Mwenyekiti wa Kamati ya Zahanati atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe walioelezwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(4) Wajumbe wa Sekretariati hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

**Taratibu za kuwapata wajumbe na muda wa kukaa madarakani**

**44** (1) Wajumbe wa Kamati ya Zahanati watachaguliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(a) Afisa Mtendaji wa Kata atatangaza nafasi wazi;

(b) Uchaguzi utafanyika kwenye Kijiji kwa njia ya mikutano ya hadhara.

(c) Mapendekezo ya majina ya wagombea yatawasilishwa kwenye Timu ya Wataalamu ya Kata ambapo yatachanganuliwa kabla ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata; na

(d) Kamati ya Maendeleo ya Kata itapendekeza majina ya wajumbe na kuyawasilisha kwenye Halmashauri kupitia kwenye Bodi ili kuidhinishwa.

(e) Kamati ya Zahanati itazinduliwa na Diwani wa kata husika.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Zahanati watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, isipokuwa kwa wajumbe ambao watashika nafasi zao kwa kupokezana, ambao watakaa kwa mwaka mmoja. Wajumbe wengine wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu na isiyozidi vipindi viwili.

**Vikao vya Kamati ya Zahanati**

**45** (1) Kamati ya Zahanati itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu isipokuwa kunaweza kukafanyika kikao cha dharura kama itahitajika.

(2) Akidi ya mkutano itakuwa ni nusu ya wajumbe wote wa kuchaguliwa ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu.

(3) Taarifa ya Kikao itatolewa kwa maandishi na Katibu, wiki moja kabla ya siku ya kikao.

**Sifa za Wajumbe**

**46** Mjumbe wa Kamati ya Zahanati anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) awe raia wa Tanzania, sharti la uraia halitawahusu wajumbe wanaotoka katika mashirika yasiyo ya kiserikali.

(b) awe na umri wa miaka ishirini na moja na kuendelea

(c) awe na elimu ya msingi au zaidi na anajua kusoma na kuandika

(d) anawakilisha watumiaji wa zahanati ;

(e) awe na akili timamu

(f) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

(g) asiwe na wadhifa wa kisiasa kutoka chama chochote cha siasa.

Kazi na majukumu ya Kamati ya Zahanati

**47.** (1). Kamati ya Zahanati itakuwa na kazi na majukumu yafuatayo:-

(a) itahakikisha kuwa jamii kwenye eneo lake inapata huduma bora na rahisi za afya;

(b) itapokea, itajadili na kupitisha mipango na bajeti ya zahanati;

(c) itatafuta na kubainisha vyanzo vya mapato ya kuendeshea huduma za Afya kwenye zahanati;

(d) itashirikiana na kamati nyingine za afya na mashirika katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya;

(e) itaendeleza miundombinu endelevu ya afya na mgao wa uhakika wa mahitaji muhimu;

(f) itashauri na kupendekeza kuhusu masuala ya watumishi yanayohusu ajira, mafunzo, mgawanyo na motisha;

(g) itasaidia na kuiwezesha Timu ya Uendeshaji ya Zahanati kupanga na kusimamia shughuli mbalimbali za jamii katika eneo lake kwa kuzingatia Mipango ya Maendeleo ya Kata;

(h) itawasilisha mipango yake ya robo mwaka, nusu mwaka na ya mwaka mzima kwenye Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri; na

(i) itafanya mambo mengine muhimu kama itakavyoagizwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

(2) Kamati ya Zahanati itawajibika kwa Bodi ya Afya ya Halmashauri.

Uhusiano na Sekta nyingine **48**. Ili kuboresha utendaji wa kazi, Kamati itakuwa na mahusiano na sekta nyingine kama ifuatavyo:-

(a) itahakikisha kuwa Jamii inawakilishwa na wajumbe kwenye Kamati ya Zahanati ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya jamii yanashughulikiwa;

(b) itapewa ushauri wa kitaalamu na Timu ya Uendeshaji wa Huduma ya Afya ya Halmashauri;

(c) itawakilishwa kwenye Kamati ya Kituo cha Afya kwa mtindo wa kupokezana ili kuhakikisha kuwa mambo ya Zahanati yanazingatiwa; na

(d) Itashirikiana na wadau wengine kwa kutafuta mapato, kujenga na kuimarisha ushirikiano.

Mapato ya Zahanati **49.** (1) Vyanzo vya mapato ya Kamati ya Zahanati vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Michango ya jamii;

(b) Mfuko wa Afya ya Jamii; (Tiba kwa Kadi)

(c) Ruzuku kutoka Halmashauri;

(d) Wahisani na washirika;

(e) Ruzuku kutoka Serikali Kuu,

(f) Mfuko wa Bima ya Afya,

(g) Gharama ya dawa/Vifaa tiba kwa asilimia hamsini (50%)

(h) Vyanzo vingine halali vya mapato.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha 1(b) ambacho mapato yake yanasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Afya ya Jamii, mapato mengineyo ya Zahanati yatahifadhiwa katika Akaunti ya zahanati na kusimamiwa na Mganga Mfawidhi wa Zahanati.

Bodi kuwa Na uwezo wa kukagua **50**. Bodi, kupitia Halmashauri, itakuwa na madaraka ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa huduma za afya zinazotolewa kwenye eneo la Halmashauri.

Makosa na **51.** Mtu yeyote ambaye:-

Adhabu

(a) atakwenda kinyume na masharti ya sheria ndogo hii; au

(b) atakayefanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi, Kamati au Timu yoyote kufanya kazi zake kwa ufanisi; au

(c ) atatumia vibaya mali na rasilimali za Bodi au Kamati na kusababisha kutofikia malengo ya Bodi;

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki moja au kifungo kwa miezi Kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.